


JINSI YULE MALAIKA

ALIVYONIJIA, NA AGIZO LAKE

 Nao hao ndugu labda ni... Ninaona vinasasauti kadhaa hapa chini, na vitanasa haya, bila shaka. Wakati wowote mnapotaka kujua aliyowaambia Roho Mtakatifu, waoneni ndugu hawa hapa ambao wana vinasasauti hivi, wanaweza kuzifungulia hizo tena, unaweza kupata haja yako hasa. Ndipo uangalie na uone kama halitukii hasa vile alivyosema Yeye, unaona. Unaposikia inapumua, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Jambo fulani, ama *hili* liko namna *hii*,’” au lichunguze tu tena na uone kama hilo ni sahihi au sivyo. Unaona? Daima liko hivyo.

² Sasa, kwa ajili ya msingi kidogo tu... Nami kwa namna fulani ninayo furaha usiku wa leo kwamba tuko wachache tu hapa. Tu jamaa wa nyumbani tu, sivyo? Sisi si, hakuna mmoja wetu, wageni. Hatuninii... Ninaweza tu kutumia sarufi yangu ya Kentucky na nijisikie niko nyumbani kabisa sasa, sababu tuko—tuko tu... Nami siitwezi Kentucky sasa, kama kuna mtu yeyote hapa kutoka Kentucky. Kuna mtu yeyote hapa kutoka Kentucky? Inua mkono wako. Loo! Ninapaswa nijisikie niko nyumbani kabisa, sivyo? Hilo ni jema sana.

³ Mama yangu alikuwa anaendesha nyumba ya kulala wageni. Nami nilishuka nikaenda huko siku moja ili nitafute... Hapo kundi kubwa la wanaume lililala humo, na ile meza kubwa na ndefu, imeandaliwa. Nami nikasema, “Ni wangapi hapa wanatoka Kentucky, simameni.” Kila mtu akasimama. Ndipo nikaenda hadi kanisani usiku huo, kanisa langu, na nikasema, “Ni wangapi hapa wanatoka Kentucky?” Kila mtu akasimama. Kwa hiyo ningesema, “Vema, hilo ni jema sana.” Wamishenari wamefanya kazi nzuri, kwa hiyo tunashukuru sana kwa jambo hilo.

⁴ Sasa, katika Kitabu cha Warumi, mlango wa 11 na kifungu cha 28. Sikilizeni kwa makini sasa kusomwa kwa Maandiko.

Basi kwa habari ya Injili, wamekuwa adui kwa ajili yenu: bali kwa habari ya kule kuchaguliwa wamekuwa wapenzi wa... kwa ajili ya baba zetu.

Kwa sababu karama na miito ya Mungu hazina majuto.

⁵ Hebu na tuombe. Bwana, tusaidie usiku wa leo sasa tunapoliendea jambo hili kwa kicho, kwa moyo wetu wote, katika unyofu, mambo haya yanasemwa tu kwa ajili ya utukufu Wako. Basi nisaidie, Bwana, na uweke tu niani mwangu mambo yale tu ambayo yanapaswa kusemwa na kiasi cha kusemwa.

Nisimamishe wakati Wako ukiwadia. Naomba kwamba kila moyo utayapokea mambo haya kwa ajili ya faida ya wagonjwa na wahitaji kwenye kusanyiko hili. Kwa kuwa ninaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁶ Sasa, ninataka kuliendea somo hili wakati tu tukiwa wachache. Na—nami nitajaribu nisiwaweke kwa muda mrefu kupita kiasi, nitaweka saa yangu hapa na kujaribu niwezavyo sasa kuwaacha mwondoke katika wakati mzuri ili muweze kurudi kesho usiku. Sasa, iweni katika maombi. Sidhani mvulana huyo hata alitoa kadi. Kamwe sikumwuliza kama yeye... Na kama hawakuzitoa au kama walizitoa ama hawakuzitoa, haijalishi. Tunazo kadi hapa ndani hata hivyo kama itatulazimu kuita baadhi. Kwa hiyo, ikiwa sivyo, mbona, tutaona tu yale Roho Mtakatifu asemayo.

⁷ Sasa, ikiwa mtasikiliza kwa makini... Sasa, hili huenda... kwa kuwa mimi... Tuko wachache tu hapa, ni wakati mzuri kusema hili, maana li—linahusika na mimi binafsi. Na hiyo ndiyo sababu nilisoma Andiko hili usiku wa leo, ili muweze kuona kwamba karama na miito si kitu chochote ambacho yeyote anaweza kustahili.

⁸ Paulo akinena hapa, alisema, “Wayahudi, katika mkondo wa Injili, walipofushwa na wakawa mbali na Mungu, nalo, ni kwa ajili yetu.” Bali kifungu kabla tu ya hicho, kilisema, “Israeli wote wataokoka.” Israeli wote wataokoka. Kulingana na kule kuchaguliwa, Mungu Baba amewapenda na amewapofusha kusudi sisi Wamataifa tuweze kupata nafasi sasa ya toba, ili kwamba, kwa njia ya Ibrahimu, Uzao wake uweze kuubariki ulimwengu wote kulingana na Neno Lake. Unaona jinsi mamlaka ya Mungu yalivyo? Neno Lake halina budi kuwa. Yeye hawezi kabisa kuwa kitu kingine. Na sasa sisi, kwa... Mungu ametuchagua sisi; amemchagua Myahudi; na Yeye ni... .

⁹ Mambo haya yote ni kutangulia kujua kwa Mungu. Alipoyatamka yale ambayo yangekuwako, Yeye alitangulia kujua hayo. Sasa, Mungu, ili awe Mungu, hapo mwanzo ilibidi Yeye ajue mwisho la sivyo hakuwa Mungu yule asiye na kikomo. Mungu hapendi kwamba yeyote apotee. La hashi! Hataki yeyote apotee. Bali katika mwanzo wa mwanzo wa siku, u—ulimwengu, Mungu alijua hasa kabisa ni nani angeokolewa na ni nani hangeokolewa. Hakutaka watu wapotee, “Si mapenzi Yake kwamba yeyote apotee, bali ni mapenzi Yake kumwokoa kila mtu,” lakini Yeye alijua tangu mwanzo ni nani angeokolewa na ni nani hangeokolewa. Hiyo ndiyo sababu angeweza kutangulia kusema, “Jambo *hili* litatukia. Jambo *lile* litatukia,” au, “*Hili* litakuwa *lile*. Mtu *huyu* atakuwa *vile*.” Mnaona?

¹⁰ Aliweza kujua kimbele kwa sababu Yeye hana kikomo. Kama unajua linalomaanisha, ni kwamba tu, “hakuna kitu Yeye asichojuu.” Unaona, Yeye anajua. Vema, hakuna kitu tangu

kabla ya wakati, na hata baada ya kutokuwepo na wakati tena, unaona, Yeye angali anajua kila kitu. Kila kitu kiko katika nia Yake. Na basi kama vile Paulo alivyosema katika Warumi, sura ya 8 na ya 9, “Basi ni kwa nini angali analaumu?” Kwa hiyo tunaona hayo, bali Mungu. . .

¹¹ Kama vile kuhubiri Injili. Mtu fulani alisema, “Ndugu Branham, unaamini Hayo?”

Nikasema, “Angalia.”

Kasema, “Wewe huna budi kuwa Mkalvinisti.”

Nikasema “Mimi ni Mkalvinisti mradi tu Kalvinisti iko katika Biblia.”

¹² Sasa, kuna tawi kwenye ule Mti, ambalo ni Ukalvinisti, lakini kuna matawi mengine zaidi kwenye huo Mti, pia. Mti una zaidi ya tawi moja. Alitaka tu kulifuatilia kule nje kufikia kwenye Usalama wa Milele, na baada ya kitambo unaingia katika wokovu wa Ulimwengu mzima kisha unaangukia kule nje mahali fulani, hakuna mwisho wake. Lakini unapomalizana na Ukalvinisti, rudi nyuma ukaanze kwenye Uarminia. Unaona, kuna tawi lingine kwenye Mti, na tawi lingine kwenye Mti, endelea tu. Kitu hicho chote pamoja kinaufanya huo Mti. Kwa hiyo ninaamini katika—katika huo. . .katika Ukalvinisti mradi tu unadumu katika Maandiko.

¹³ Nami ninaamini ya kwamba Mungu alijua kabla ya msingi wa ulimwengu, akalichagua Kanisa Lake katika Kristo, na akamchinja Kristo kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu. Maandiko yalisema hivyo, “Alikuwa Mwana-kondoo wa Mungu aliyechinjwa kabla ya msingi wa ulimwengu.” Unaona? Naye Yesu alisema ya kwamba Yeye alitujua kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, Paulo alisema ya kwamba, “Yeye—Yeye alitujua na akatangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo kabla ya ulimwengu kuumbwa.” Huyu ni Mungu. Huyu ni Baba yetu. Unaona?

¹⁴ Kwa hiyo usiwe na wasiwasi, magurudumu yanazunguka sawasawa kabisa, kila kitu kinakuja katika wakati wake. Jambo pekee, ni, ingia katika mzunguko. Na hiyo ndiyo—hiyo ndiyo sehemu iliyo nzuri kuhusu hilo, ndipo unajua jinsi ya kutenda kazi unapoingia katika huo mzunguko.

¹⁵ Sasa, angalieni sasa, “Karama na miito bila majuto,” hiyo ndiyo njia ya pekee ambayo ningeweza—ningeweza Kimaandiko kuuweka mwito wangu katika Bwana. Nami natumaini kwamba nipo pamoja na marafiki usiku wa leo ambao hakika wataelewa jambo hili na wasilifikirie kuwa la kibinafsi, bali kwamba mweze kuwa na ufahamu na kujua tu yale—yale ambayo Bwana amesema kwamba Yeye angetenda, nanyi mwone jambo fulani linaloendelea na kisha mlifuate.

¹⁶ Sasa, hapo mwanzo, kitu cha kwanza ambacho ninaweza kukumbuka ni ono. Kitu cha kwanza ambacho ninaweza kukikumbuka akilini mwangu ni ono ambalo Bwana alinipa. Na hiyo ilikuwa miaka mingi, mingi iliyopita, nilikuwa mvulana mdogo sana. Nami nilikuwa na jiwe mkononi mwangu.

¹⁷ Sasa, samahani, ninaweza kukumbuka nilipokuwa ninavaa gauni refu. Sijui iwapo ninyi (yeyote wenu ninyi nyote) mlio na umri wa kutosha kukumbuka wakati wavulana wadogo walipokuwa wakivaa magauni marefu. Ni wangapi humu ndani wanakumbuka wakati watoto walipovaa, naam, magauni marefu? Vema, naweza kukumbuka, kwenye kibanda changu kidogo cha kale tulipokuwa tunaishi, nilikuwa ninatambaa sakafuni. Na ilikuwa ni mtu fulani, sijui ilikuwa ni nani, akaingia. Na Mama alikuwa ametengeneza maskini—maskini mkanda wa samawati katika vazi langu. Basi nilikuwa tu hata siwezi kutembea vizuri. Bali nilikuwa ninatambaa wakati huo, na nikakita kidole changu katika theluji iliyokuwa kwenye miguu yao, na nilikuwa nikila hiyo theluji kutoka miguuni mwake huku amesimama karibu na jiko, akijipasha moto. Namkumbuka mama yangu akinivuta niondoke kwa sababu ya hiyo.

¹⁸ Na halafu jambo lingine ninalokumbuka, hapana shaka lilikuwa yapata miaka miwili baadaye, nilikuwa na jiwe dogo. Na hiyo ingenifanya mwenye umri wa kama miaka mitatu, na kaka yangu mdogo wakati huo angekuwa tu hajafikia kabisa umri wa miaka miwili. Na basi tulikuwa huko nje nyuma ya uga ambako kulikuwa na uga wa zamani wa kuchanja ambako walikuwa wakileta kuni na kuzichanja kuni. Ni wangapi wanazikumbuka siku hizo mlipokuwa mnazikokota kuni nyuma ya uga na kuzichanja? Kwa nini hata nikavaa tai usiku wa leo? Ni—niko nyumbani kabisa.

¹⁹ Basi wakati wao... Nje huko kwenye huo uga wa kale wa kuchanja kuni kulikuwako na tawi dogo lililoinama chini huko, likitokea kwenye ile chemchemi. Tulikuwa na maskini kata ya kibuyu huko kwenye chemchemi ambako tungechota maji yetu na kuyaweka kwenye maskini hiyo ndoo, ndoo ya zamani ya mwerezi, na kuishusha.

²⁰ Nakumbuka mara ya mwisho nilipomwona maskini nyanya yangu, kabla ya kufariki, alikuwa na umri wa miaka mia moja na kumi. Na wakati alipofariki, nilimchukua mikononi mwangu na kumshikilia hivi kabla tu ya kufariki. Alinikumbatia, na kusema, “Mungu aibariki nafsi yako, mpenzi, sasa na milele,” wakati alipofariki.

²¹ Na sidhani mwanamke huyo aliwahi kuwa na jo—jozi moja ya viatu vyake mwenyewe, maishani mwake. Pia nakumbuka nikimwangalia, na hata wakati nilipokuwa kijana mwanamume, ningeshuka niende nikawaone, kila asubuhi angeamka, miguu

mitupu, na kupitia kwenye theluji ile hadi kwenye chemchemi, achote ndoo ya maji na kurudi, miguu yake moja kwa moja ndani ya hiyo. Kwa hiyo haikudhuru, aliishi akafikia umri wa miaka mia moja na kumi. Kwa hiyo (ndiyo, bwana) alikuwa na mwili mshupavu sana, sana, pia.

²² Hivyo basi ninakumbuka alitaka kuniambia kuhusu gololi za baba yangu alizokuwa akichezea alipokuwa mvulana. “Na maskini kizee hicho,” nikawazia, “atapandaje huko darini?” Kibanda kidogo cha kale, chenye vyumba viwili, na kilikuwa na orofa ndogo huko juu. Nao walikuwa wamekata miti miwili midogo, kisha wakatengeneza ngazi, ya kupandia juu. Vema, nikasema...

²³ Vema, sasa, akasema, “Sasa, baada ya chakula cha kutwa nitakwambia, nitakuonyesha go—gololi za baba yako.”

Nami nikasema, “Vema.”

²⁴ Kwa hiyo alikuwa anaenda kunionyesha hizo, katika kasha orofani alimokuwa ameweka vikorokoro vyake kama wafanyavyo wazee. Ndipo nikawaza, “Maskini kizee kile atapandaje ile ngazi?” Kwa hiyo nilisogea karibu pale nikasema, “Nyanya,” nikasema, “sasa, ngoja, mpenzi, nitapanda juu hapa nikusaidie.”

²⁵ Akasema, “Simile.” Akapanda ngazi hiyo kama kuchakulo. Akasema, “Vema, njoo!”

Nami nikasema, “Sawa, Nyanya.”

²⁶ Nikawaza, “Loo, jamani, laiti ningeliweza tu kuwa namna hiyo, niwe ningali na kiasi hicho cha nguvu ndani yangu kwenye umri wa miaka mia moja na kumi!”

²⁷ Sasa, ndipo ninakumbuka nikiwa kwenye chemchemi hii ndogo ya zamani, nami nilikuwa na jiwe na nilikuwa nikilitupa chini namna hiyo, kwenye matope, nikijaribu kumwonyesha kaka yangu mdogo jinsi nilivyokuwa na nguvu. Na kulikuwa na ndege aliyeketi juu kwenye mti naye alikuwa akilia kwa mlio mwembamba, akirarua kila mahali, maskini robini mdogo ama kitu fulani. Na, maskini robini huyo, nilifikiri alizungumza na mimi. Ndipo nikageuka na kusikiliza, naye ndege huyo akaruka na kuenda zake, na Sauti ikasema, “Utaishi sehemu kubwa ya maisha yako karibu na mji uitwao New Albany.”

²⁸ Hiyo ni maili tatu toka mahali nilipolelewa. Kaenda, kama mwaka mmoja baadaye, mpaka mahali pale, bila ya kuwa na hata wazo la kuwahi kwenda... New Albany. Kote kupitia maishani, jinsi mambo hayo...

²⁹ Sasa, angalia, watu wangu hawakuwa wa kidini. Baba na mama yangu hawakwenda kanisani. Kabla ya hapo, walikuwa Wakatoliki.

³⁰ Maskini mpwa wangu anayeketi hapa ndani mahali fulani usiku wa leo, nadhani, sijui. Yeye ni mwanajeshi. Ninamwombea.

Yeye mwenyewe ni Mkatoliki, bado ni Mkatoliki. Na jana jioni, wakati alipokuwa hapa na kuona mambo hayo ya Mungu, alikuwa amesimama pale pale jukwaani. Alisema, akisimama pale, basi akasema, “Uncle Bill?” Amekuwa nchi za ng’ambo kwa muda mrefu, kasema, “Nilipoona hayo...” Kasema, “Hayo—hayo hayatendeki katika kanisa la Katoliki.” Akasema, “Hayo... Na—naamini, Uncle Bill, uko sahihi,” akasema.

³¹ Na kwa hiyo nikasema, “Mpenzi, si *mimi* niliye sahihi, ni Yeye aliye sahihi. Unaona, Yeye ndiye aliye sahihi.” Na kwa hiyo akasema yeye... nikasema, “Sasa, sikuombi ufanye chochote, Melvin, bali mtumikie tu Bwana Yesu Kristo kwa moyo wako wote. Wewe nenda popote utakapo. Bali uwe na hakika kwamba moyoni mwako kwamba Yesu Kristo amekwisha kuzaliwa upya, unaona, moyoni mwako. Ndipo uende kwenye kanisa lolote unalotaka baada ya jambo hilo.”

³² Sasa, lakini watu walionitangulia walikuwa Wakatoliki. Baba yangu ni Muairishi na mama yangu alikuwa Muairishi. Pengo dogo tu lililopo katika damu ya Kiairishi, nyanya yangu alikuwa Mhindi wa Cherokee. Mama yangu ni karibu tu chotara. Na kwa hiyo basi mimi... kwangu mimi, ni ninii yangu... kizazi chetu, baada ya cha tatu kimetoweka. Lakini hilo ndilo pengo pekee katika kuwa Muairishi halisi, Harvey na Branham ndilo lililokuwa jina. Na halafu nyuma ya hayo lilikuwepo Lyons, ambalo lingali ni la Kiairishi. Na basi wote walikuwa Wakatoliki. Bali mimi mwenyewe, hatukuwa na malezi yoyote ya dini au mafundisho hata kidogo, tukiwa watoto.

³³ Lakini karama hizo, hayo maono, niliona maono wakati uo huo kama vile tu niyaonavyo sasa, hiyo ni kweli, kwa sababu karama na miito havina majuto. Ni kutangulia kujua kwa Mungu, Mungu akitenda jambo fulani. Kote katika maisha nilikuwa ninaogopa kusema lolote kuhusu jambo hilo.

³⁴ Mmesoma hadithi yangu katika kitabu kidogo kiitwacho *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*. Nafikiri kiko katika baadhi ya vitabu, hivi vingine. Hiyo ni kweli, Gene? Kiko katika hiki, kitabu cha kawaida—cha kawaida, katika kile—katika kile kitabu tulicho nacho sasa? Ni, *Hadithi ya Maisha*? Nafikiri ndicho. Basi tulipokuwa... Hivi hilo si ni jambo baya sana? Vitabu vyangu mwenyewe, na kamwe sijavisoma, mwenyewe. Lakini mtu mwingine huviandika, kwa hiyo basi ni kitu fulani tu wamechukua katika mkutano. Nimepitia hilo, kwa hiyo ninatazamia jambo lingine sikuzote kutukia. Kwa hiyo, basi, ni vizuri, nimesoma visehemu-sehemu vyake sasa, hapa na pale, ninapopata tu nafasi.

³⁵ Na sasa, kwa vyovyote, kama—kama mvulana mdogo, mnajua lile ono jinsi lilivyonena nami, nilikuwa na umri wa kama miaka saba, na kasema, “Usinywe pombe wala kuvuta sigara wala kuchafua mwili wako kwa njia iwayo yote,

kutakuwa na kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima.” Nanyi mmelisikia hilo likisimuliwa katika kitabu. Vema, hilo ni kweli. Wakati wote liliendelea kutukia.

³⁶ Nilipofanyika mhudumu, vema, basi hilo—basi hilo lilianza hasa kutukia wakati wote.

³⁷ Nami usiku mmoja nikamwona Bwana wetu Yesu. Ninasema hili kwa kibali, ninaamini, kutoka kwa Roho Mtakatifu. Yule Malaika wa Bwana ambaye huja siye Bwana Yesu. Hafanani na Yeye katika ono lile lile. Kwa kuwa, ono nililoona la Bwana Yesu, Yeye alikuwa Mtu mdogo. Yeye hakuwa . . . nilishakuwa huko nje uwanjani, nikimwomba baba yangu. Nami nilirudi ndani na kwenda kitandani, na usiku huo nilimtazama na ni—nikasema, “Ee Mungu, mwokoe!”

³⁸ Mama yangu ameokolewa tayari na nilikuwa nimembatiza. Basi nikawaza, “Loo, baba yangu hunywa pombe kweli.” Ndipo nikawaza, “Laiti ningaliweza tu kumfanya amkubali Bwana Yesu!” Nikatoka nje, nikalala kwenye mto mdogo wa nyasi nje kwenye chumba cha mbele, karibu na mlango.

³⁹ Na Kitu fulani kikaniambia, “Inuka.” Ndipo nikainuka, nikaanza kutembea, na nikarudi kule uwanjani nyuma yangu, uwanja wa zamani wa manyasi.

⁴⁰ Na hapo, akisimama si zaidi ya futi kumi kutoka kwangu, palisimama Mtu; amevaa vazi jeupe, Jamaa mdogo; amekunja mikono Yake namna *hii*; ndevu, kwa namna fulani ni mfupi; nywele zimefika mabegani Mwake; na Yeye alikuwa akiangalia kando kutoka kwangu, namna *hiyo*; akionekana mtu mwenye amani. Bali sikuweza kuelewa na jambo hilo, jinsi miguu Yake, mmoja ukiwa nyuma tu ya mwingine. Na upepo ukivuma, vazi Lake likipepea, manyasi yakitikiswa na upepo.

⁴¹ Nikawaza, “Sasa, ngoja kidogo.” Nikajiuma. Nikasema, “Sasa, siko usingizini.” Na nikavuta chini, nikavuta na kuondoa kipande kidogo cha hayo manyasi, mwajua, nikakata kama kijipande cha kuchokolea meno. Nikakiingiza kinywani mwangu. Nikaangalia nyuma kuelekea nyumbani. Nikasema, “La, nilikuwa ndani mle nikimwomba baba, ndipo Kitu fulani kikasema njoo huku nje, na hapa Mtu huyu amesimama.”

⁴² Nikawaza, “Huyo anaonekana kama Bwana Yesu.” Nikawaza, “Sijui kama ndiye?” Alikuwa anaangalia pale pale kabisa, moja kwa moja kuelekea mahali nyumba yetu ilipo sasa. Kwa hiyo nikazunguka upande *huu* kuona kama ningeweza kumwona. Nami niliweza kuona upande wa uso Wake namna *hiyo*. Bali Yeye . . . Ilinibidi kuzunguka upande namna *hii* ili kumwona. Ndipo nikasema, “Uhum!” Kamwe hakusogea. Nami nikawaza, “Naamini nitamwita.” Basi nikasema, “Yesu.” Na alipofanya hivyo, aligeuka na kuangalia namna *hiyo*. Hayo tu ndiyo ninayokumbuka, alinyosha tu mikono Yake.

⁴³ Hakuna msanii duniani angeweza kuchora picha Yake, sifa za uso Wake. Ile iliyo bora kuliko zote niliyowahi kuona ni ile ya *Kichwa cha Kristo Akiwa na Miaka Thelathini na Mitatu* iliyochorwa na Hofmann, ninayo kwenye vitabu vyote na kila kitu ninachotumia. Hiyo ni kwa sababu hiyo huonekana kama tu ndiyo yenyewe, na hivyo basi... au karibu kabisa, karibu iwezavyo kuwa.

⁴⁴ Alionekana kama, Mtu, iwapo angenena, ulimwengu ungalikwisha, na hata hivyo akiwa mwenye upendo mwingi na wema mpaka u—u... nilianguka tu. Na mchana, nilijikuta tu kwenye mapambazuko, shati la pajama likiwa limelowa kwa machozi, nilipordia fahamu zangu, nikitembea, kupitia uwanja ule wa manyasi, kurudi nyumbani.

⁴⁵ Nilimwelezea rafiki yangu mhudumu. Akasema, “Billy, Hilo litakufanya mwendawazimu.” Akasema, “Huyo ni ibilisi.” Tena kasema, “Usicheze na kitu kama hicho.” Nilikuwa mhudumu wa Kibaptisti wakati huo.

⁴⁶ Vema, nilikwenda kwa rafiki yangu mwingine wa zamani. Nikaketi chini na kumwelezea kuhusu Hilo. Nikasema, “Ndugu, unaonaje juu ya Hilo?”

⁴⁷ Akasema, “Vema, Billy, nitakwambia.” Akasema, “Naamini kama ungejaribu kuyahifadhi maisha yako, hubiri tu kilichoko hapa kwenye Biblia, neema ya Mungu na kadhalika, nisingeyaendea mazingaombwe fulani, jambo la namna hiyo.”

⁴⁸ Nikasema, “Bwana, simaanishi kufuatilia mazingaombwe fulani.” Nikasema, “Jambo tu ninalojaribu kutafuta kujua ni kile hiki kilicho.”

⁴⁹ Akasema, “Billy, miaka mingi iliyopita walikuwa na mambo hayo makanisani. Lakini,” kasema, “mitume walipokoma, mambo hayo yalikoma pamoja nao.” Kisha kasema, “Sasa kitu pekee tulicho nacho ambacho... namna yoyote ya kuyaona mambo hayo,” kasema, “ni wanaowasiliana na mizimu, pepo.”

Nikasema, “Loo, Ndugu McKinney, unamaanisha hilo?”

Akasema, “Naam, bwana.”

Nikasema, “Ee Mungu, nirehemu!”

⁵⁰ Nikasema, “Mimi—mimi... Loo, Ndugu McKinney, uta—utajiunga nami katika maombi ili Mungu alizuie lisinifanyikie kamwe? Unajua nampenda nami sitaki kukosea katika mambo haya.” Nikasema, “Omba pamoja nami.”

⁵¹ Akasema, “Nitaomba, Ndugu Billy.” Na kwa hiyo tulifanya maombi pale pale katika—katika nyumba ya mchungaji.

⁵² Niliwauliza wahudumu kadha. Jambo lile lile lingekuja. Basi niliogopa kuwauliza, sababu wangenifikiria mimi kuwa ni ibilisi. Kwa hiyo si—sikutaka kuwa hivyo. Nilijua moyoni mwangu kitu fulani kilitukia. Sasa, ni hayo tu, kulikuwa—

kulikuwa na kitu moyoni mwangu ambacho kilitendeka. Na sikutaka kuwa hivyo, kamwe.

⁵³ Kwa hiyo baadaye katika miaka mingi, nilisikia siku moja huko chini kwenye kanisa la Wabaptisti wa Kwanza ambako nilikuwa mshirika wakati huo, nilimsikia mtu fulani akisema, “Aisee, laiti ungeenda kule na kuwasikia wale watakatifu wanaobingirika jana usiku.”

⁵⁴ Nami nikawaza, “Watakatifu wanaobingirika?” Na rafiki yangu, Walt Johnson, mwimbaji besi, nami nikasema, “Hicho kilikuwa ni kitu gani, Ndugu Walt?”

Akasema, “Kundi la hawa Wapentekoste.”

Nikasema, “Ati nini?”

⁵⁵ Akasema, “Wapentekoste!” Kasema, “Billy, kama ungeona hilo,” kasema, “walikuwa wanabingirika sakafuni namna hiyo na kurukaruka.” Kisha akasema, “Walisema ya kwamba iliwabidi kupayuka katika lugha isiyojulikana au ha—hawakuwa wameokolewa.”

Nami nikasema, “Ni wapi huko?”

⁵⁶ “Loo,” kasema, “mkutano mdogo wa kizamani wa hema nje huko, upande ule mwingine wa Louisville.” Kasema, “Watu weusi, bila shaka.”

Ndipo nikasema, “A-ha.”

Naye akasema, “Kuna wazungu wengi huko.”

Nikasema, “Walifanya hivyo, pia?”

Kasema, “Ndiyo, ndiyo! Walifanya hivyo, pia.”

⁵⁷ Nikasema, “Hilo ni jambo la kushangaza, watu wanachanganyikiwa katika mambo ya namna hiyo.” Nikasema, “Vema, nadhani inatubidi tu kuwa na mambo hayo.” Jumapili moja asubuhi, sitaisahau kamwe. Alikuwa anakula ganda kavu la chungwa kwa sababu ya tumbo kuvimba, nami naweza tu kuliona jambo hilo vema kabisa kama kwamba ilikuwa ni jana. Nami nikawaza, “Kupayukapayuka, kurukaruka, watakata dini ya aina gani baada ya hiyo?” Na kwa hiyo ni—nikaendelea.

⁵⁸ Baadaye kutoka hapo, nilikutana na mzee mmoja ambaye yupo hapa kanisani labda sasa, ama alikuwepo hapa kanisani, kwa jina la John Ryan. Nami nilimkuta mahali fulani... Maskini jamaa mwenye ndevu ndefu na nywele, na huenda yupo hapa. Nilifikiri alitoka Benton Harbor huku juu, kwenye House of David.

⁵⁹ Nao walikuwa na mahali huko Louisville. Nilikuwa ninajaribu kuwatafuta watu hao, nao walipaita Shule ya Manabii. Kwa hiyo nikafikiri ningeenda huko na kuona ni nini hiyo. Vema, sikuona mtu yeyote akibingirika sakafuni, lakini walikuwa na mafundisho mageni. Na hapo ndipo nilipokutana na mzee huyu, yeye alinalika niende kwake.

⁶⁰ Nilipanda nikaenda huko kwa likizo. Ndipo nilikuwa huko siku moja, na nikarudi nyumbani kwake naye alikuwa ametoka, na alikuwa ameenda mahali fulani huko Indianapolis. Kasema, “Bwana alimwita,” mke wake.

Nikasema, “Unamaanisha unamwachilia mtu huyo arandarande tu namna hiyo?”

⁶¹ Akasema, “Loo, yeye ni mtumishi wa Mungu!” Maskini mwanamke huyo alikufa majuma machache yaliyopita, nasikia. Naye alikuwa amejitolea sana kwa huyo mume. Jamani, hiyo ndiyo aina ya mwanamke unayepaswa kuwa naye! Hiyo ni kweli. Awe sawa ama awe makosani, yu sahihi hata hivyo! Nikasema . . . Vema, nilijua wao . . .

⁶² Sasa yeye . . . Ndugu Ryan, upo hapa? Hayupo hapa. Alikuwepo hivi majuzi, sivyo, wavulana?

⁶³ Vema, wanaishi tu kwa kile wanachoweza kupata, naye hakuwa na chochote cha kula nyumbani. Hiyo ni kweli. Nami nilikuwa nimevua samaki wachache huko kidimbwini, ama ziwani, huko Michigan, nami nikashuka nikarudi—nami nikashuka nikarudi mahali pale. Nao hata hawakuwa na shahamu humo nyumbani, ama mafuta, kupikia samaki. Nami nikasema, “Amewaacha bila ya kitu chochote nyumbani?”

Kasema, “Loo, lakini yeye ni mtumishi wa Mungu, Ndugu Bill!” Kasema, “Yeye . . .”

⁶⁴ Nami nikawaza, “Vema, ubarikiwe maskini moyo wako. Ndugu, nitasimama na wewe moja kwa moja.” Hiyo ni kweli. “Unawazia kiasi hicho kuhusu mume wako, mimi niko tayari kuungana na kushikamana nawe kwa ajili ya jambo hilo.” Hiyo ni kweli. Tunahitaji wanawake wengi zaidi wa namna hiyo leo hii, na wanaume wengi zaidi wanaofikiria juu ya wake zao namna hiyo. Hiyo ni kweli. Ingekuwa Marekani bora zaidi kama waume na wake wangeungana pamoja namna hiyo. Wawe sawa ama makosani, kaa nao. Kusingalikuwako na talaka nyingi.

⁶⁵ Kwa hiyo tu—tulienda . . . Halafu nikaendelea. Basi njiani nikienda nyumbani, lilikuwa jambo la ajabu, niliteremka kupitia Mishawaka. Nami nikaona maskini—maskini motokaa kuukuu sasa, zimeegeshwa barabarani, jina lake . . . maandishi makubwa-makubwa juu yao yaliyosema, “Yesu Pekee.” Nikawaza, “Hivi ni nini . . . ‘Yesu Pekee,’ hilo lazima ni la kidini.” Nami nikaenda upande huu na hapa kuna baiskeli zilizokuwa zimeandikwa hivyo, “Yesu Pekee.” Makadilaki, Ford Muundo wa T, kila kitu, kimeandikwa “Yesu Pekee.” Nikawaza, “Vema, nashangaa hicho ni kitu gani?”

⁶⁶ Kwa hiyo nikalifuatilia; nikaja kugundua, ulikuwa ni mkutano wa dini, watu elfu moja na mia tano hadi elfu mbili hapo. Ndipo nikasikia huko kupaza sauti kwote na kurukaruka, na kuendelea. Nikawaza, “Labda, hapa ndipo nitakapoona kile walicho watakatifu wanaobingirika.”

⁶⁷ Kwa hiyo nilikuwa na Ford yangu kuukuu, mwajua, ambayo nilidai ingekwenda maili thelathini kwa saa, kumi na tano upande *huu* na kumi na tano juu chini upande *huu*. Kwa hiyo nikaiegsha upande mmoja, ni... nilipopata mahali pa kuegeshea, kisha nikaenda zangu barabarani. Nikaingia, nikaangalia huku na huku, na kila mtu amesimama ambaye angeweza kusimama. Ilinibidi kutazama juu ya vichwa vyao. Nao walikuwa wanapiga mayowe, na kuruka, na kuanguka, na kupiga makelele. Nikawaza, “Whiu, umhu, ni watu wa namna gani hawa!”

⁶⁸ Bali nilivyoziidi kusimama pale, ndivyo nilivyoziidi kujisikia vizuri. Nikawaza, “Hilo linaonekana ni jambo jema mno.” Nikawaza, “Hakuna kasoro yoyote kwa hao watu. Hawana kichaa.” Nikaanza kuzungumza na baadhi yao, kwa hiyo wao—wao walikuwa ni watu wazuri. Basi nikasema...

⁶⁹ Vema, sasa, huo ndio mkutano ule ule ambao nilitoka nikaenda na kukaa usiku kucha usiku huo, na siku iliyofuata nikaingia. Nanyi mmesikia nikisimulia hayo katika hadithi ya maisha yangu. Nilikuwa jukwaani pamoja na wahudumu mia moja na hamsini, ama mia mbili, na labda zaidi, nao walitaka kila mtu ainuke tu na kusema walikotoka. Nami nikasema, “Mwinjilisti William Branham, Jeffersonville,” nikaketi, “Mbaptisti,” kwa hiyo, nikaketi. Kila mmoja alisema anatoka wapi.

⁷⁰ Kwa hiyo asubuhi hiyo iliyofuata nilipoingia mle... nililala uwanjani usiku kucha usiku huo, na kunyosha suruali yangu katikati ya viti viwili vya ile Ford, mwajua, na mimi—mimi... suruali chakavu yenye milia, maskini fulana ya mikono, unajua. Kwa hiyo asubuhi iliyofuata nikaenda mkutanoni, nimevaa maskini fulana yangu ya mikono. Nilikuwa nimekwenda...

⁷¹ Sikuwa na chochote ila dola tatu, na nilikuwa nipate petroli ya kutosha kufika nyumbani. Ndipo basi ni—nikanunua sambusa, ile ya aina ya kale, mwajua, lakini nilikuwa sawa. Basi nilifika kwenye bomba la maji, nikajichotea glasi moja ya maji, mwajua, na yalikuwa mazuri sana. Kwa hiyo nilikuwa nimezilowesha kidogo, ndipo nikapata kifungua kinywa.

⁷² Sasa, ningeweza kula pamoja nao, sasa, wao hula mara mbili kwa siku. Bali sikuweza kuweka kitu chochote kwenye sadaka, kwa hiyo nisinge—nisingewanyonya wao.

⁷³ Kwa hiyo basi mimi—basi nikaingia humo asubuhi ile, wakasema...yanibidi tu nisimulie sehemu hii ya kisa hicho. Ndipo basi nikaingia humo asubuhi ile, nao wakasema, “Tunamtafuta William Branham, mwinjilisti kijana aliyekuwa jukwaani jana usiku, Mbaptisti.” Kasema, “Tunamtafuta yeye alete ujumbe asubuhi hii.” Niliona lilikuwa linaenda kunivuta sana, kundi hilo la watu, mimi nikiwa Mbaptisti. Kwa hiyo kwa namna fulani nikainama tu chini hapo kwenye kiti changu.

Nilikuwa nimevaa suruali yenye milia na fulana ya mikono; mwajua, na sisi tulivaa kikasisi, kwa hiyo...Nami niliketi nyuma kwenye kiti namna hii. Kwa hiyo aliuliza mara mbili ama tatu. Nami niliketi karibu na ndugu mweusi.

⁷⁴ Na sababu ya wao kufanya mkutano wao huko Kaskazini, kwa sababu ubaguzi ulikuwa unaendelea huko Kusini wakati huo. Kwa hiyo hawangeweza kuufanyia huko Kusini.

⁷⁵ Basi nilishangaa hii “Yesu Pekee” ilihusu nini. Nami nikawaza, “Mradi tu ni Yesu, ni sawa. Kwa hiyo haileti tofauti yoyote kama ni... jinsi ilivyo, mradi tu ni Yeye.”

⁷⁶ Kwa hiyo niliketi pale kidogo na kuwaangalia, na kwa hiyo wakaita mara mbili ama tatu zaidi. Ndipo huyu ndugu mweusi akaniangalia, akasema, “Je! unamjua?” Ni—ni—ni... Changamoto ilikuwa pale. Singeweza kumdanganya mtu huyo, sikutaka kufanya hivyo.

Nikasema, “Angalia, ndugu. Ndiyo, ninamjua.”

Akasema, “Vema, nenda ukamwite.”

⁷⁷ Nikasema, “Vema, ni—nitakuambia, ndugu,” nikasema, “mimi ndiye. Lakini, unaona,” nikasema, “angalia, mimi... suruali hii yenye milia.”

“Panda uende kule.”

⁷⁸ Nami nikasema, “La, siwezi kwenda kule,” nikasema, “na suruali hii niliyovaa, namna hii, maskini fulana hii ya mikono.”

Kasema, “Hao watu hawajali unavyovalia.”

⁷⁹ Ndipo nikasema, “Vema, angalia, usiseme hilo. Unasikia?” Nikasema, “Unaona, nimevaa suruali hii yenye milia, sitaki kupanda kwenda kule.”

Kasema, “Yeyote anayejua alipo William Branham?”

Akasema, “Huyu hapa! Huyu hapa!”

⁸⁰ Loo, jamani! Uso wangu mwekundu kwelikweli, mwajua; na bila ya tai, mwajua; na maskini fulana hii ya mikono kuukuu, mwajua, na mikono mifupi ya shati namna hii. Nami nilikwenda ninapita kule, huku masikio yangu yanawaka moto. Sijawahi kamwe kuwapo penye maikrofoni.

⁸¹ Na basi nikaanza kuhubiri pale juu, ndipo nikachukua somo, kamwe sitalisahau, “Yule tajiri aliyainua macho yake kuzimuni, na ndipo akalia.” Mimi, mara nyingi, huhubiri mambo madogo matatu namna hiyo, “Njoni muone mtu,” “Je! unayasadiki hayo?” au “Ndipo akalia.” Nami niliendelea kusema, “Hakuna maua, na ndipo akalia. Hakuna mikutano ya maombi, ndipo akalia. Hakuna watoto, ndipo akalia. Hakuna nyimbo, ndipo basi akalia.” Halafu nikalia.

⁸² Kwa hiyo baada ya yote kumalizika, mbona, jamani, wakawa tu... wote wamenizunguka, wakinitaka niende nikawahubirie kwenye mkutano. Ndipo nikawaza, “Aisee, huenda mimi

ni mtakatifu anayebingirika!” Unaona? Kwa hiyo nikawaza, “Huenda ikawa . . .” Unaona? Walikuwa ni watu wazuri sana.

⁸³ Basi nikatoka nikaenda huko nje. Mwanamume aliyevaa jozi ya buti za cowboy, na kofia kubwa ya cowboy, nikasema, “Wewe ni nani?”

Akasema, “Mimi ni Mzee *Fulani-wa-fulani* kutoka Texas.”

Nikawaza, “Vema, hiyo ilionekana . . .”

⁸⁴ Jamaa mwingine akaja amevaa hizi suruali ndogo-ndogo na pana za aina ya kufungiwa magotini, mwajua, walizocheza nazo gofu, na moja ya hizo sweta ndogo nzito. Akasema, “Mimi ni Kasisi *Fulani-wa-fulani* kutoka Florida. Naomba uje ukafanye . . .”

⁸⁵ Nikawaza, “Niko nyumbani kabisa, jamani, nikivalia hii suruali yenye milia na fulana ya mikono. Hilo ni barabara kabisa.”

⁸⁶ Kwa hiyo, mmesikia hadithi ya maisha yangu juu ya mambo hayo, kwa hiyo nitakomea hapa na kuwaelezea jambo fulani ambalo sijawahi kulisimulia hapo kabla. Jambo la kwanza, nataka kuwaulizeni . . . Nilikuwa ninaenda kuliacha hilo. Sijawahi kulisema hapo kabla hadharani, maishani mwangu. Kama mtaniahidi ya kwamba mnanipenda na mtajitahidi kunipenda vile vile baada ya mimi kusema jambo hili kama mliyoniipenda kabla sijalisema, inua mkono wako. Vema. Hiyo ni ahadi yenu, nitawashikilieni kwayo.

⁸⁷ Nikiwa nimeketi mkutanoni usiku ule, walipokuwa wanaimba nyimbo zao wakipiga makofi. Nao wangeimba, “Na . . .” Wimbo ule mfupi, “Najua ilikuwa ni ile Damu. Najua ilikuwa ni ile Damu.” Nao wangekimbia huku na huko kwenye marefu, na kila kitu, huku wanapaza sauti tu na kumsifu Bwana. Nikawaza, “Hilo linasikika ni zuri sana kwangu.” Nikaanza . . .

⁸⁸ Nao walikuwa wakirejea wakati wote kwenye Matendo, Matendo 2:4, Matendo 2:38, Matendo 10:49, yote hayo. Nikawaza, “Aisee, hayo ni Maandiko! Nilikuwa tu sijawahi kuliona jambo Hilo namna hiyo hapo kabla.” Bali, loo, moyo wangu ulikuwa unawaka, kawaza, “Hili ni zuri mno!” Nilidhania walikuwa kundi la watakatifu wanaobingirika nilipokutana nao mara ya kwanza, ndipo nikawaza, “Loo, jamani! Sasa wao ni kundi la malaika.” Mnaona, nikabadilisha mawazo yangu haraka sana.

⁸⁹ Basi asubuhi iliyofuatia Bwana alipokuwa amenipa nafasi hii muhimu kufanya mikutano hii, nikafikiri, “Loo, jamani, nitaambatana na kundi hili la watu! Haina budi hao ni aina ya wale waliozoea kuwaita ‘Wamethodisti wanaopiga kelele.’ Kasonga tu mbele kidogo,” nikawaza. “Pengine ndio hao.” Basi nikawaza, “Vema, mimi . . . mimi hakika napenda jambo

hilo. Loo, kuna kitu fulani kuwahusu ninachokipenda, wao ni wanyenyekevu na wapole.”

⁹⁰ Kwa hiyo jambo moja nisingeweza kuelewa ni kule kunena kwa lugha, huko kulinisumbua. Na mimi... Kulikuwa na mtu mmoja, tuseme, akiketi *hapa* na mmoja *hapa*, nao ndio walikuwa viongozi wa lile kundi. *Huyu* angeinuka na kunena kwa lugha, *huyu* angeifasiri nao wangetoa habari za mambo kuhusu mkutano na kadhalika. Nikafikiri, “Jamani, whiu, lazima niyasome hayo!” Hivyo basi wangebadiilishana, anashuka juu ya *huyu* na kisha anarudi juu ya *yule*; na kila mmoja angenena kwa lugha, afasiri. Wengine wao kanisani wangenena, bali haikuonekana kama kwamba tafsiri ilikuja kama ya watu hawa wawili. Sasa, niliona waliketi karibu-karibu, nikawaza, “Loo, jamani, lazima hao wawe ni Malaika!” Kwa hiyo nilipokuwa nimeketi nyuma kule...

⁹¹ Chochote hicho kilichokuwa (mwajua) nisingeweza kukifahamu, kingekuwa juu yangu. Nami ninayo njia ya kujua mambo kama Bwana anataka mimi niyajue, mwajua. Nami si... Hiyo ndiyo sababu nasema silitoi hili nje, kamwe sijawahi kulitoa hadharani hapo kabla. Kama kweli ninataka kujua kitu chochote, Bwana kwa kawaida huniambia kuhusu mambo haya. Hiyo ndiyo kazi ya hiyo karama, mnaona. Kwa hiyo huwezi mkuitupa tu hicho mbele za watu, inakuwa kama kutupa lulu zako mbele ya nguruwe. Ni kitu wakfu, kitakatifu, nawe hutaki kufanya hivyo. Kwa hiyo, Mungu angeniwajibisha. Kama vile kuzungumza na ndugu na kadhalika, nisingejaribu kutafuta jambo ovu kumhusu ndugu.

⁹² Wakati mmoja nikiwa nimeketi mezani na mtu fulani, amenikumbatia kwa mkono wake, kasema, “O Ndugu Branham, nakupenda.” Na nikaendelea kuhisi kitu fulani kikisogea. Nikamtazama. Asingeweza kuniambia hilo; nilijua hakunipenda, unaona, kwa sababu hapo lilijitokeza. Alikuwa mnafiki kabisa, kama kuliwahi kuweco na mmoja, mnaona, na papo hapo akiwa amenikumbatia.

⁹³ Nikasema, “Vema, sawa,” nikaondoka. Sitaki kujua hilo. Afadhali nimjue tu vile ninavyomjua, kama ndugu yangu, na kuliacha liende namna hiyo. Nimwache Mungu afanye yale yaliyobaki. Mnaona? Nami sitaki ku... sijui, sitaki kujua mambo hayo.

⁹⁴ Na mara nyingi katika mambo haya, si hapa kanisani. Nitakuwa nimeketi chumbani, nimeketi mkahawani, na Roho Mtakatifu ataniambia mambo yatakayotukia. Watu wapo papa hapa ambao wanajua hilo kuwa ni kweli. Nitaketi nyumbani kwangu nami nitasema, “Sasa, iweni waangalifu, kuna motokaa itakayokuja baada ya kitambo kidogo. Itakuwa ni mtu *fulani-fulani*. Waleteni ndani, kwa maana Bwana amesema watakuwa hapa.” “Tutakaposhuka kwenda barabarani, kutakuwa na

mambo *fulani* yatakayotukia. Kuwa mwangalifu kwenye kile kivuko pale, kwa sababu nusura utagongwa.” Na kuona tu kama sivyo ilivyo, unaona, kila wakati, kikamilifu tu! Kwa hiyo hutaki kujiingiza sana kwenye mambo hayo, kwa sababu ungeninii... Ni—ni... Unaweza kukitumia, ni kipawa cha Mungu, lakini inakubidi uangalie unafanya nini nacho. Mungu atakuwajibisha.

⁹⁵ Mwangalie Musa. Musa alikuwa mtu aliyetumwa na Mungu. Unaamini jambo hilo? Aliyechaguliwa kimbele, akakusudiwa tangu zamani, na kufanywa nabii! Basi Mungu akamtuma huko, kasema, “Nenda ukanene na mwamba,” baada ya huo kupigwa. Kasema, “Nenda ukanene na mwamba, nao utatoa maji yake.”

⁹⁶ Lakini Musa, akiwa na hasira, akaenda huko mbio akaupiga ule mwamba. Maji hayakutoka, akaupiga tena, kasema, “Enyi waasi! Ni lazima tuwatolee maji katika mwamba huu?”

⁹⁷ Unaona alichokifanya Mungu? Maji yalitoka, bali kasema, “Panda huku juu, Musa.” Huo ndio ulikuwa mwisho wake, mnaona. Yakupasa kuwa mwangalifu na mambo hayo, kwa hiyo wewe... unachotenda na vipawa vya Mungu.

⁹⁸ Kama vile tu mhubiri, mhubiri mzuri na hodari, akitoka na kuhubiri kwa madhumuni tu ya kukusanya sadaka na fedha, Mungu atamfanya awajibikie hilo. Hiyo ni kweli. Inakupasa uwe mwangalifu kile unachofanya na vipawa vya Mungu. Na, ama unajaribu kujitengenezea hadhi fulani ama jina kubwa kwa ajili ya kanisa fulani, ama jina kubwa kwa nafsi yake. Afadhali niwe na mkutano wa siku mbili au tatu usiku na kuendelea mahali pengine, na niwe mnyenyekevu, na niketi chini. Na mnajua yale ninayomaanisha. Naam, bwana, daima jiweke mahali ambapo Mungu anaweza kuweka mkono Wake juu yako.

Haya ni Maisha ya ndani sasa, kumbuka.

⁹⁹ Kwa hiyo basi siku hii, nikawaza, “Vema, nitapanda niende kule.” Nami nilikuwa nimeshtushwa sana na wale watu, nikawaza, “Nitachunguza habari za watu hao.” Na huko uwanjani nilikaza kuwatafuta baada ya ibada kwisha. Nilitazama huku na huko. Nikampata mmoja wao, nikasema “U hali gani, bwana?”

¹⁰⁰ Akasema, “Sijambo!” Kasema, “Wewe ndiwe yule kijana mhubiri aliyehubiri asubuhi ya leo?”

Nikasema... Nilikuwa na umri wa miaka ishirini na mitatu wakati huo. Nikasema, “Ndiyo, bwana.”

Naye akasema, “Jina lako lilikuwa ni nani?”

Nikasema, “Branham.” Kisha nikasema, “Lako?”

¹⁰¹ Naye akaniambia jina lake. Nami nikawaza, “Vema, sasa, kama ningeweza tu kupata mawasiliano na roho yake sasa.” Na hata hivyo bila kujua ni kitu gani kilikuwa kinatenda jambo hilo.

Ndipo nikasema, “Vema, aisee, bwana,” nikasema, “ninyi watu mnacho Kitu fulani hapa ambacho sina.”

Akasema, “Je! umempata Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?”

Nikasema, “Vema, mimi ni Mbaptisti.”

¹⁰² Akasema, “Lakini je! umempokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?”

¹⁰³ Nami nikasema, “Vema, ndugu, unamaanisha nini?” Nikasema, “Si—sina kile mliche nacho ninyi nyote, najua hilo!” Nikasema, “Kwa sababu mnacho Kitu fulani kinachoonekana kuwa na nguvu na kwa hiyo . . .”

Kasema, “Umewahi kunena kwa lugha?”

Nami nikasema, “La, bwana.”

Kasema, “Nitakwambia mara moja huna Roho Mtakatifu.”

¹⁰⁴ Basi nikasema, “Vema, kama mimi . . . Kama hicho ndicho kinahitajika kumpata Roho Mtakatifu, mimi sina.”

¹⁰⁵ Na kwa hiyo akasema, “Vema, kama hujanena kwa lugha, hunaye.”

¹⁰⁶ Na kuendeleza mazungumzo yake namna hiyo, nikasema, “Vema, nitampata wapi?”

¹⁰⁷ Kasema, “Ingia chumbani mle na uanze kumtafuta Roho Mtakatifu.”

¹⁰⁸ Nami nikaendelea kumwanguka, mwajua. Hakujuu kile nilichokuwa nikifanya, lakini yeye . . . nilijua alikuwa na hisi ndogo isiyo ya kawaida, sababu yeye . . . macho yake yalianza kuwa meupe kidogo alipokuwa akinitazama. Naye . . . Lakini yeye alikuwa Mkristo kweli. Alikuwa kabisa, asilimia mia moja juu ya alama, Mkristo. Hiyo ni kweli. Vema, nikawaza, “Mungu asifiwe, Hili hapa! Ya—ya—yanipasa kwenda kwenye madhabahu yale mahali fulani.”

¹⁰⁹ Nikatoka, nikatazama pande zote, nikawaza, “Nitamtafuta yule mtu mwingine.” Na nilipompata na nikaanza kuzungumza naye, nilisema, “Hujambo, bwana?”

¹¹⁰ Akasema, “Hivi, wewe ni wa kanisa gani?” Akasema, “Wananiambia wewe ni Mbaptisti.”

Nikasema, “Naam.”

Naye akasema, “Hujampata Roho Mtakatifu bado, sivyo?”

Nikasema, “Vema, sijui.”

Kasema, “Umewahi kunena kwa lugha?”

Nikasema, “La, bwana.”

Kasema, “Huna.”

111 Nami nikasema, “Vema, najua sina kile mlichio nacho nyinyi nyote. Najua hilo.” Kisha nikasema, “Lakini, ndugu yangu, kwa kweli ninakihitaji Hicho.”

Akasema, “Vema, kile—kile pale kidimbwi, tayari.”

112 Nikasema, “Nimebatizwa. Lakini,” nikasema, “si—sijapokea kile nyinyi nyote mlichio nacho.” Nikasema, “Mnacho kitu fulani ambacho na—nakitaka sana.”

Naye akasema, “Vema, hilo ni sawa.”

113 Nilikuwa nikijaribu kumshika, unaona. Na kama ni... Hatimaye nilipoipata roho yake, sasa, huyo alikuwa yule mtu mwingine, kama niliwahi kuzungumza na mnafiki duni kwelikweli, ndiye huyo hapo mmoja wao! Alikuwa anaishi... Mke wake alikuwa mwanamke mwenye nywele nyeusi, yeye alikuwa anaishi na mwanamke mwenye nywele za rangi ya shaba na alikuwa amezaa watoto wawili naye. Anakunywa pombe, analaani, anakwenda kwenye vilabu, na kila kitu kingine, na bado yuko humo ndani na ananena kwa lugha na kutabiri.

114 Kisha nikasema, “Bwana, nisamehe.” Nikaenda nyumbani. Hiyo ni kweli. Nikasema, “Nitachukua tu... Siwezi kuelewa na jambo hilo. Ilionekana kama Roho Mtakatifu mbarikiwa anashuka, na, juu ya huyo mnafiki.” Nikasema, “Haiwezekani! Hivyo tu.”

115 Kwa kipindi hiki kirefu basi, mimi nikisoma na kulia, nikawaza kama ningeweza kutoka niambatane nao labda ningeweza kuona haya yote yalikuwa yanahusu nini. Huyu hapa mmoja, Mkristo halisi; na yule mwingine, mnafiki kwelikweli. Ndipo nikawaza, “Ni nini basi? Loo,” nikasema, “Mungu, labda—labda kuna kasoro fulani kwangu mimi.” Nami nikasema, mimi nikiwa mtu wa kimsingi, “Hiyo ita... itabidi nione hilo katika Biblia. Lazima.”

116 Kwangu mimi, kila kitu kinachofanya kazi lazima kitoke kwenye Biblia hii la sivyo si sahihi. Lazima kitoke Hapa. Kinaweza kuthibitishwa katika Biblia, si mahali pamoja tu, bali hakina budi kitoke kote katika Biblia. Sina budi kukiamini. Lazima kifungamane na kuumana na kila Andiko la sivyo sikiamini hicho. Halafu basi, kwa sababu Paulo alisema, “Kama malaika kutoka Mbinguni akija, akihubiri injili nyingine yoyote, na alaaniwe.” Kwa hiyo ninaamini Biblia.

Ndipo nikasema, “Singeweza kamwe kuona kitu kama hicho katika Biblia.”

117 Miaka miwili baadaye, baada ya kumpoteza mke wangu na kila kitu, nilikuwa kule kwenye Green's Mill, mahali pangu padogo pa zamani kule juu, nikiomba. Nilikuwa nimerudi kwenye pango langu nyuma kule kwa siku mbili ama tatu, ilikuwa siku mbili. Nilitoka nje nipate kupunga hewa kidogo, nipate hewa kidogo. Basi nilipokwenda huko, Biblia yangu

ilikuwa imekaa huko mwishoni mwa gogo unapoingia tu. Mti mmoja wa kale uliangushwa na upepo, ulikuwa na tawi panda. Sasa, wewe... Ulikuwa na tawi panda lililokaa namna *hii*, na ule mti umeanguka chini. Nami niliketi tu kwa kutagaa lile gogo, nikalala huko wakati wa usiku, nikiangalia juu kuelekea angani namna hiyo, mkono wangu ukiwa juu namna *hii*, na wakati mwingine naingia usingizini nimelala barabara kwenye gogo namna hiyo, nikiomba. Niko huko siku kadhaa, sili wala sinywi, nipo hapo tu nikiomba. Nami nilitoka nje kwenda kupata hewa safi kidogo, nje ya lile pango; kulikuwa na baridi, unyevunyevu nyuma huko ndani.

¹¹⁸ Kwa hiyo basi nikatoka na hapo ilikaa Biblia yangu ambapo niliiweka siku iliyotangulia, na ilikuwa imefunguliwa kwenye Waebrania, mlango wa 6. Ndipo nikaanza kusoma hapo, “Na tuweke kando... mwendo... tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu, tusiweke tena msingi wa kuzitubia kazi zisizo na uhai na wa kuwa na imani kwa Mungu,” na kadhalika. “Kwa maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa kipawa cha mbinguni, na miito,” na kadhalika. Bali kasema, “Bali miiba na michongoma ambayo iko karibu na kukataliwa, ambayo mwisho wake... maji... mvua hunya juu ya nchi mara kwa mara kuilowesha na kuitayarisha kwa hao ambao—hao ambao wako karibu kukataliwa, pamoja na miiba na michongoma, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.”

Ndipo Kitu fulani kikafanya, “Whoooooossh!”

¹¹⁹ Nikawaza, “Hii hapa. Nitasikia sasa hivi lolote Yeye... Aliniamsha usingizini hapa, anatararisha kunipa ono sasa hivi.” Nikangojea hapo mwishoni mwa gogo lile, na kungojea. Nikasimama na kutembea huku na huko, juu chini. Nikarudi, hakuna kitu kilichotukia. Nikarudi pangoni mwangu tena, hakuna kitu kilichotukia. Nilisimama pale, nikawaza, “Vema, ni nini hii?”

¹²⁰ Nikaenda kwenye Biblia yangu tena, na, loo, Hilo likanijia kote tena. Nikaichukua, ndipo nikawaza, “Mna kitu gani humo Yeye anachotaka nikisome?” Nikaendelea kusoma kuhusu “toba kwa Mungu, na imani,” na kadhalika, na nikaendelea kusoma ambapo ilisema, “Mvua huja mara kwa mara juu ya nchi kuilowesha na kuiandaa kwa kile kilichokusudiwa, kwa kuwa hapa, bali miiba na michongoma iliyo karibu na kukataliwa ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.” Na, loo, Hilo lingenitetemesha tu!

¹²¹ Na nikawaza, “Bwana, utanipa ono la kile...” Nilikuwa huko juu kumwomba Yeye kitu kingine.

¹²² Ndipo mara ghafla, mbele yangu, niliona dunia ikizunguka, na yote ilikuwa imelimwa. Na hapa akatokea mtu aliyevaa nguo nyeupe, amekiinua kichwa chake, anapanda Mbegu namna hii. Basi alipoondoka, akija, mara tu alipopanda kile kilima, hapa

akaja mtu nyuma yake, amevaa mavazi meusi, ameinamisha kichwa chake, anapanda mbegu. Na zile Mbegu njema zilipomea, ilikuwa ni ngano; na zile mbegu mbaya zilipomea, ilikuwa magugu.

¹²³ Na halafu kukaja ukame mkubwa juu ya nchi, na ngano ikaning'iniza kichwa chake, karibu iangamie, ikihitaji maji. Nami niliwaona watu wote wameinua mikono yao juu, wakimwomba Mungu alete maji. Na halafu nikaona lile gugu, lilikuwa limeinamisha kichwa chake, limeinama kwa ajili ya maji. Na mara tu yale mawingu makubwa yakatokea na mvua ikamwagika. Na ilipofanya hivyo, maskini ile ngano iliyoinama kabisa ikafanya, "Whish," ikasimama wima. Na maskini lile gugu karibu nayo likafanya, "Whish," likasimama wima.

Nikawaza, "Vema, ni nini hicho?"

¹²⁴ Ndipo likanijia. Hilo hapo. Mvua ile ile inayoifanya ngano kukua, hufanya gugu kukua. Na Roho Mtakatifu yule yule anayeweza kushuka katika kundi la watu, naye anaweza kumbariki mnafiki kama vile tu anavyombariki yule mwingine. Yesu alisema, "Kwa matunda yao mtawajua." Sio kama anapaza sauti, kama anashangilia, bali "ni kwa matunda yake mtamjua."

¹²⁵ Nikasema, "Haya basi!" "Nimelipata, Bwana." Nikasema, "Basi hiyo hasa ndiyo Kweli." Mtu huyu . . . Ungeweza kuwa na vipawa bila ya kumjua Mungu.

¹²⁶ Kwa hiyo basi mimi—basi nilikuwa ninakosoa sana kunena kwa lugha, unaona. Lakini siku moja, basi, jinsi Mungu alivyolithibitisha hilo kwangu!

¹²⁷ Nilikuwa nikibatiza huko mtoni, waongofu wangu wa kwanza, kwenye Mto Ohio, na mtu wa kumi na saba niliyekuwa nikimbatiza, nilipoanza kumbatiza, nilisema, "Baba, ninapombatiza kwa maji, Wewe umbatize na Roho Mtakatifu." Nikaanza ku—kumwingiza majini.

¹²⁸ Na mara tu basi kisulisuli kikaja toka juu mbinguni, na hapa ikaja hiyo Nuru, ikiangaza chini. Mamia na mamia ya watu wakiwa ukingoni, saa nane kamili za mchana, mwezi wa Juni. Nayo ikaning'inia papo hapo juu ya mahali nilipokuwa. Sauti ikanena kutoka hapo, ikasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa awe mtangulizi wa kuja kwa kwanza kwa Kristo, wewe unao . . . unao Ujumbe utakaoleta kule kutangulia kwa Kuja kwa Pili kwa Kristo." Na hilo liliniogopesha nusura kufa.

¹²⁹ Ndipo nikarudi nyuma, na watu wote pale, wa—wafanya kazi wa kiwanda cha chuma na wote wale, mwuza dawa, na hao wote waliokuwa ukingoni. Nilikuwa nimebatiza karibu mia mbili au mia tatu alasiri hiyo. Nao waliponitoa, waliponivuta kutoka majini, mashemasi na wengineo wakapanda juu, wakaniuliza, kasema, "Nuru hiyo ilimaanisha nini?"

¹³⁰ Kundi kubwa la watu weusi waliotoka kwenye—kwenye kanisa la Baptisti la Gilt Edge na kanisa la Lone Star kule chini, na wengi wa hao waliokuweco huko chini, walianza kupiga mayowe walipoyaona hayo yakitukia, watu wakazimia.

¹³¹ Msichana fulani niliyejaribu kumfanya aondoke hapo kwenye mashua, akiwa ameketi pale huku amevaa suti ya kuogelea, mwalimu wa shule ya Jumapili kwenye kanisa fulani, nami nikasema, “Hivi hutaondoka, Margie?”

Akasema, “Billy, si lazima nitoke.”

¹³² Nikasema, “Hiyo ni kweli, si lazima utoke, lakini ningekuwa na heshima ya kutosha kwa ajili ya Injili kutoka mahali ninapobatizia.”

Akasema, “Si lazima nitoke.”

¹³³ Na wakati alipokuwa ameketi pale, akicheka kwa dhihaka na kunicheka wakati nikibatiza, maana hakuamini katika kubatiza, kwa hiyo basi Malaika wa Bwana aliposhuka alianguka kifudifudi humo ndani ya mashua. Leo hii huyo msichana yuko kwenye hospitali ya wendawazimu. Kwa hivyo huwezi tu kumchezea Mungu. Unaona? Sasa, baadaye... Msichana mrembo, alianza kunywa pombe baadaye, akapigwa na chupa, chupa ya—ya bia, ikamkatakata uso mzima. Loo, mtu mwenye sura ya kuchukiza sana! Na likatukia hapo.

¹³⁴ Na halafu maishani mwote ningeyaona hayo, ninaona hilo likisonga mbele, ninaona maono hayo, vile mambo hayo yangetukia. Halafu, baadaye kidogo, Hilo liliendelea kunitatiza sana, na kila mtu akiniambia Hilo lilikuwa ni makosa. Nami nikaondoka kwenda kwenye kambi yangu ya zamani, huko juu ambako mara zote niliomba hata nikajibiwa. Na ninge... Haidhuru ningeendelea kuomba kiasi gani kwa ajili ya Jambo hilo lisinijie, lilikuja hata hivyo. Na kwa hiyo basi nilikuwa tu... nilikuwa—nilikuwa mlinzi wa wanyama pori katika Jimbo la Indiana. Basi nikaingia, palikuwa na mtu aliyeketi pale, kakake mpiga piano wangu kwenye maskani. Naye akasema, “Billy, utaambatana nami kwenda huko Madison alasiri ya leo?”

Nikasema, “Siwezi kufanya hivyo, yanibidi niende huko mbugani.”

¹³⁵ Nami ningeninii... nikaja tu karibu na nyumba na kuvua mshipi wangu, mshipi wa bunduki na kadhalika, na kukunja mikono ya shati langu. Tuliishi katika nyumba ndogo yenye vyumba viwili, nami nilikuwa ninaenda kunawa ili kujitayarisha kwa ajili ya chakula changu. Basi nilikuwa nimekwisha nawa, na ninatembea tu kuzunguka karibu na nyumba, chini ya m—mti mkubwa wa mtakawa, na mara ghafla Kitu fulani kikafanya, “Whooooosssh!” Nami karibu tu nizimie. Ndipo nikaangalia, nikajua ni kile Kitu tena.

¹³⁶ Nikaketi kwenye hivyo vipandio, naye akaruka kutoka kwenye motokaa yake akanikimbilia, kasema, “Billy, unazimia?”

Nikasema, “La, bwana.”

Akasema, “Kuna nini, Billy?”

¹³⁷ Nami nikasema, “Sijui.” Nikasema, “Endelea tu, ndugu, hilo ni sawa. Asante.”

¹³⁸ Mke wangu akatoka nje akaniletea gudulia la maji, akasema, “Mpenzi, kuna nini?”

Nikasema, “Hakuna kitu, mpenzi.”

¹³⁹ Kwa hiyo akasema, “Njoo sasa, chakula cha kutwa kiko tayari,” naye akanikumbatia kwa mkono wake, akajaribu kuniingiza ndani.

¹⁴⁰ Nikasema, “Mpenzi, na—nataka kukwambia jambo fulani.” Nikasema, “Wewe wapigie simu uwaambie sitakuwoko huko alasi hii.” Nikasema, “Meda, mpenzi,” nikasema, “ninajua moyoni mwangu nampenda Yesu Kristo. Najua ya kwamba nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Lakini sitaki ibilisi awe na uhusiano wowote na mimi.” Kisha nikasema, “Siwezi kuendelea namna hii; mimi ni mfungwa.” Nikasema, “Mara zote, jambo hili linapoendelea kutukia, mambo kama hayo, na maono haya kuja, na kadhalika namna hiyo. Ama, chochote kile,” nikasema, “hunifanyikia.” Sikujua lilikuwa ni ono. Sikuliita ono. Nikasema, “Hivyo vitu kama mpagao,” nikasema, “Sijui hilo ni nini. Pia, mpenzi, si—si—si—sitaki kucheza nalo, wa—wananiambia ni ibilisi. Nami nampenda Bwana Yesu.”

¹⁴¹ “Loo,” akasema, “Billy, hupaswi kusikiliza yale watu wanayokwambia.”

¹⁴² Nikasema, “Lakini, mpenzi, waangalie wahubiri wengine.” Nikasema, “Si—sikitaki kitu hicho.” Nikasema, “Ninaenda mahali pangu msituni. Nina karibu dola kumi na tano, wewe mtunze Billy.” Billy alikuwa mvulana mdogo sana wakati huo, jamaa mdogo sana. Nikasema, “Wewe—wewe chukua... Hizo zinakutosha wewe na Billy kuishi kwazo, kwa kipindi kidogo. Wapigie simu uwaambie nita—nitarudi labda kesho, na naweza nisirudi kabisa. Ikiwa sikurudi katika siku tano zijazo, waweke nitu mahali pangu.” Kisha nikasema, “Meda, sitatoka kamwe kwenye msitu huo mpaka Mungu aniahidi ataniondolea kitu hicho na asikiruhusu kutukia tena.” Wazia upumbavu mtu anaoweza kuwa nao!

¹⁴³ Nami nikapanda nikaenda huko usiku huo. Nikarudi kule kwenye maskini kile kibanda, kabla ya siku iliyofuata; kidogo muda ulikuwa umeenda. Nilikuwa niende hadi kwenye kambi yangu siku iliyofuata, juu kwenye...mbele zaidi karibu na mlima, ama kilima, hasa, na kupanda huko msituni. Siamini F.B.I. wangeweza kunipata kule juu. Kwa hiyo kibanda hiki

kidogo cha zamani . . . Nilikuwa nikiomba aduhuri hiyo yote na kabla hakujakuwa na giza sana. Ningeomba, nilikuwa nikisoma pale katika Biblia paliposema, “Roho za manabii humtii nabii.” Sikuweza kulielewa hilo. Basi kukawa giza sana katika maskini kibanda hicho cha kale.

¹⁴⁴ Mahali nilipokuwa nikiinasia nilipokuwa mvulana, nilikuwa na ugwe wa kutegea mahali pale, na kuenda huko juu na kuvua samaki na kukaa usiku kucha. Maskini kibanda kidogo tu cha kale ambacho kimechakaa na kimekaa hapo, kimekuwa huko ndani kwa miaka kadhaa. Mpangaji fulani huenda aliishi humo kabla hakijafikia hali hiyo.

¹⁴⁵ Na kwa hiyo ni—nilikuwa tu nangojea pale. Ndipo nikafikiri, “Vema.” Ikafikia karibu saa saba, saa nane, saa tisa asubuhi, nilikuwa ninatembea huku na huko sakafuni, nikienda huku na huko. Ninaketi kwenye stuli ndogo ya kale pale, ndogo . . . si stuli, kijisanduku cha zamani cha kitu fulani. Basi nikaketi chini pale, na nikawaza, “Ee Mungu, kwa nini Wewe unitendee haya?” Nikasema, “Baba, Wewe unajua ninakupenda. Wewe unajua ya kwamba ninakupenda! Na si—si—sitaki kupagawa na ibilisi. Sitaki mambo hayo yanipate mimi. Tafadhali Mungu, usiyaruhusu yatendeke tena.”

¹⁴⁶ Nikasema, “Na—nakupenda. Sitaki kwenda kuzimuni. Kuna faida gani mimi kuhubiri na kujaribu, na kuweka juhudi zangu, ikiwa niko makosani? Nami sijipeleki mwenyewe tu kuzimuni, ninawaongoza maelfu ya wengine vibaya.” Ama, mamia ya wengine, katika siku hizo. Kisha nikasema . . . Nilikuwa na huduma kubwa. Tena nikasema, “Vema, si—sitaki hilo linifanyikie tena.”

¹⁴⁷ Basi nikaketi kwenye hii stuli ndogo. Nami nimeketi tu, loo, kwa namna fulani nimekaa hivi, namna *hiyo* tu. Ndipo, mara ghafla, nikaona Nuru ikimemetesha humo chumbani. Nami nikafikiri kuna mtu aliyekuwa anakuja na tochi. Ndipo nikatazama huku na huku, na nikafikiri, “Vema . . .” Na hapa ikatokea, moja kwa moja mbele zangu. Na sakafu ya zamani ya mbao. Basi Hiyo hapo, moja kwa moja mbele zangu. Ni stovu ndogo ya pipa iliyokuwa pembeni, sehemu yake ya juu haipo. Na—na papa *hapa* ndani palikuwa na Nu—Nuru sakafuni, ndipo nikawaza, “Vema, hiyo iko wapi? Vema, hiyo haingekuwa inakuja. . .”

¹⁴⁸ Nikatazama kote. Nayo Hii hapa juu yangu, Nuru ii *hii*, pale pale juu yangu, ikining’inia moja kwa moja namna *hiyo*. Ikizungukazunguka kama moto, kidogo ina rangi ya zumaridi, ikifanya, “Whoossh, whoossh, whoossh!” namna hiyo, juu Yake tu, namna hiyo. Nami nikaitazama Hiyo. Nikawaza, “Ni nini Hiyo?” Sasa, Hiyo ilinitisha mno.

¹⁴⁹ Nikasikia mtu akija, [Ndugu Branham anaigiza mtu anayetembea—Mh.] akitembea tu, ila tu, alikuwa miguu mitupu.

Ndipo nikaona mguu wa Mtu ukiingia. Ilikuwa giza chumbani, kote isipokuwa hapa ambapo Hiyo ilikuwa inaangazia papo hapo chini. Basi nikaona mguu wa Mtu ukiingia. Basi wakati alipoingia mle chumbani, akaja anatembea, alikuwa Mtu apataye... alionekana kuwa na uzito wa kama ratili mia mbili. Alikuwa amekunja mikono Yake namna *hii*. Sasa, nilikuwa nimeiona Hiyo kwenye Upepo wa Kisulisuli, nilikuwa nimeshaisikia ikinena nami, na nikaiona Hiyo katika umbo la Nuru, bali ni mara ya kwanza niliyowahi kuona sura Yake. Ikaja kwangu, karibu sana.

¹⁵⁰ Vema, kweli marafiki, ni—nilidhani moyo wangu utasimama. Ni... Hebu fikiria! Jiweke mwenyewe pale, ingekufanya ujisikie vivyo hivyo. Pengine umesonga mbali zaidi safarini kuliko mimi, labda umekuwa Mkristo kwa muda mrefu zaidi, lakini ingekufanya ujisikie namna hiyo. Maana baada ya mara mamia na mamia ya kunitembelea, inanifanya nife ganzi hapo anaponikaribia. Wakati mwingine hata inanifanya... karibu nizimie kabisa, mnyonge kabisa ninapoondoka jukwaani mara nyingi. Kama nikikaa sana, nitazimia kabisa. Nimewafanya wanizungushe katika motokaa kwa saa nyingi, bila ya hata kujua nilikuwa wapi. Nami siwezi kulielezea. Someni hapa chini kwenye Biblia, nayo italielezea Hilo, ni kitu gani. Maandiko yanasema hivyo!

¹⁵¹ Kwa hiyo nilikuwa nimeketi hapo na kumwangualia. Kwa—kwa namna fulani nilikuwa nimeinua mkono wangu juu namna *hiyo*. Alikuwa akinitazama moja kwa moja, wa kupendeza sana. Bali alikuwa na Sauti nzito kwelikweli, na Yeye akasema, “Usiogope, nimetumwa kutoka Uweponi mwa Mwenyezi Mungu.” Na aliponena, Sauti hiyo, hiyo ilikuwa ndiyo Sauti ile ile iliyonena nami nilipokuwa na umri wa miaka miwili, koteke nikikua. Nilijua huyo alikuwa ni Yeye. Na nikawaza, “Sasa...”

¹⁵² Basi lisikilizeni. Sasa yasikilizeni yale mazungumzo. Nitayanukuu vizuri niwezavyo, nijuavyo, neno kwa neno, maana nisingekumbuka vizuri.

¹⁵³ Yeye... Nikasema... Nilimtazama namna hiyo. Akasema, “Usiogope,” kwa utulivu tu, kasema, “Nimetumwa kutoka Uweponi mwa Mwenyezi Mungu, kukuambia ya kwamba kuzaliwa kwako kwa ajabu...” Kama mjuavyo vile kuzaliwa kwangu kulivyokuwa kule juu. Nuru iyo hiyo ilining’inia juu yangu nilipozaliwa kwanza. Basi kwa hiyo akasema, “Kuzaliwa kwako kwa ajabu na maisha yako yasiyoeleweka yamekuwa ni kuonyesha ya kwamba unapaswa kwenda ulimwenguni kote na kuwaombea wagonjwa.” Kisha kasema, “Na bila kujali wana nini...” Naye alitaja. Mungu, Yule aliye Hakimu wangu, anajua. Kwamba, alitaja “kansa.” Kasema, “Hakuna chochote... Kama ukiwafanya watu wakuamini, na uwe mnyofu unapoomba,

hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako, si hata kansa.” Mnaona, “Kama ukiwafanya watu wakuamini wewe.”

¹⁵⁴ Basi nikaona hakuwa adui wangu, alikuwa Rafiki yangu. Nami sikujua kama—kama nilikuwa ninakufa au nini kilikuwa kikifanyika wakati alipokuwa akinijia hivyo. Nami nikasema, “Vema, Bwana,” nikasema, “Mimi ni...” Nilijua nini kuhusu kuponya na mambo kama hayo, karama hizo? Nikasema, “Vema, Bwana, mimi ni... mimi—mimi ni mtu maskini.” Kisha nikasema, “Niko miongoni mwa watu wangu. Na—naishi na watu wangu ambao ni maskini. Sina elimu.” Halafu nikasema, “Na ni—ni—nisingeweza, hawata—hawatanielewa.” Nikasema, “Wao—hawata—hawatanisikiliza.”

¹⁵⁵ Naye akasema, “Kama vile nabii Musa alivyopewa vipawa viwili, ishara,” hasa, “ili kuthibitisha huduma yake, vivyo hivyo utapewa viwili—vivyo hivyo umepewa vipawa viwili kuthibitisha huduma yako.” Akasema, “Kimoja cha hivyo kitakuwa kwamba utamshika mkono mtu unayemwombea, kwa mkono wako wa kushoto na wao wa kulia,” halafu kasema, “halafu usimame tu kimya, na itakuwa... kutakuwa na tukio la maumbile litakalotukia mwilini mwako.” Kisha kasema, “Halafu uombe. Na kikitoweka, huo ugonjwa umeondoka kwa watu hao. Kisipotoweka, omba tu baraka na uende zako.”

“Vema,” nikasema, “Bwana, nahofia hawatanipokea.”

¹⁵⁶ Akasema, “Na jambo la pili litakuwa, kama hawatasikia hilo, basi watasikia hili.” Kasema, “Ndipo itakuwa kwamba utajua siri yenyewe ya moyo wao.” Kasema, “Hili watasikia.”

¹⁵⁷ “Vema,” nikasema, “Bwana, hiyo ndiyo sababu nipo hapa usiku wa leo. Nimeambiwa na makasisi wangu ya kwamba mambo hayo ambayo yamekuwa yakinijia ni makosa.”

¹⁵⁸ Akasema, “Ulizaliwa ulimwenguni humu kwa kusudi hilo.” (Mnaona, “karama na mwito havina majuto.”) Akasema, “Ulizaliwa ulimwenguni humu kwa kusudi hilo.”

¹⁵⁹ Ndipo nikasema, “Vema, Bwana,” nikasema, “hicho, makasisi wangu waliniambia hicho, ya kwamba hicho kilikuwa ni ro—roho mwovu.” Tena nikasema, “Wao... Hiyo ndiyo sababu nipo hapa nikiomba.”

¹⁶⁰ Na haya hapa yale aliyoninukulia. Alinielezea juu ya kuja kwa Bwana Yesu, katika mara Yake ya kwanza. Nami nikasema...

¹⁶¹ Kitu cha ajabu kilikuwa, marafiki... Vema, nitasimama papa hapa kwa dakika moja tu, nirudi nyuma. Kilichonifanya niogope kuliko nilivyowahi kuogopa, kila nilipokutana na mpiga ramli, wagnetambua kuna jambo lililokuwa limetukia. Na hilo lingenini tu... nusura liniue.

¹⁶² Kwa mfano, siku moja mimi na binamu zangu tulikuwa tunateremka kupitia u—uwanja wa sherehe, nasi tulikuwa

wavulana tu, tukitembea pale. Basi palikuwa na maskini mpiga ramli aliyekuwa ameketi pale kwenye moja ya mahema hayo, msichana, msichana mwenye sura nzuri, alikuwa ameketi pale. Nasi sote tulikuwa tukienda, tunatembea karibu na mahali pale. Akasema, "Aisee, wewe, njoo hapa kidogo!" Na sisi wavulana watatu tukageuka. Naye akasema, "Wewe uliye na sweta yenye milia." Huyu alikuwa ni mimi.

¹⁶³ Nami nikasema, "Ndiyo, mama?" Nilidhania ya kwamba yeye pengine alitaka kunituma nikamletee Coke, au kitu fulani kingine cha namna hiyo. Naye alikuwa mwa—mwanamke kijana, labda akiwa na umri wa miaka ya mapema ya ishirini, ama kitu fulani, ameketi pale. Nami nikaenda pale, nikasema, "Ndiyo, mama, nikufanyie nini?"

¹⁶⁴ Naye akasema, "Aisee, hivi ulijua kuna Nu—Nuru inayokufuata? Ulizaliwa chini ya ishara fulani."

Nikasema "Unamaanisha nini?"

¹⁶⁵ Akasema, "Vema, ulizaliwa chini ya ishara fulani. Kuna Nuru inayokufuata. Ulizaliwa kwa ajili ya mwito wa Kiungu."

Nikasema, "Toka hapa, ewe mwanamke!"

¹⁶⁶ Nikaanza kwenda zangu, kwa sababu mama yangu daima aliniambia mambo ya namna hiyo yalikuwa ni ya ibilisi. Alikuwa sahihi. Kwa hiyo mimi . . . Hilo lilinitisha.

¹⁶⁷ Na siku moja nilipokuwa mlinzi wa wanyama pori, nilikuwa ninasafiri kwenye basi. Basi nikaingia kwenye basi. Sikuzote ilionekana kama kwamba ninaandamwa na roho. Nilikuwa nimesimama pale, naye baharia huyu alikuwa amesimama nyuma yangu. Nami nilikuwa ninaenda kule kwenye doria, nami nilikuwa ninaenda kwenye Mbuga za Henryville, nalikuwa kwenye basi. Niliendelea kuhisi kitu fulani kisicho cha kawaida. Nikatazama kote pale, na kulikuwa na mwanamke m—mkubwa mnene ameketi pale, amevalia vizuri. Akasema, "U hali gani?"

Nikasema, "Sijambo!"

¹⁶⁸ Nilifikiria alikuwa ni mwanamke tu, mwajua, anazungumza, kwa hiyo nikaendelea tu. . . Akasema, "Ningetaka kuzungumza na wewe kidogo."

Nikasema, "Ndiyo, mama?" Nikageuka.

Akasema, "Hivi ulijua ya kwamba ulizaliwa chini ya ishara?"

¹⁶⁹ Nikafikiri, "Mwingine wa hao wanawake wa ajabu." Kwa hiyo nikaendelea tu kuangalia nje. Na kwa hiyo sikusema neno, niliendelea tu. . .

¹⁷⁰ Akasema, "Naweza kuzungumza na wewe kwa dakika moja?" Nikaendelea tu. . . Akasema, "Usijifanye namna hiyo."

¹⁷¹ Nilikaza tu kutazama mbele. Nikawaza, "Huo si uungwana."

Akasema, "Ningependa kuzungumza nawe kwa muda mfupi tu."

¹⁷² Nikaendelea tu kuangalia mbele, na sikumjali hata kidogo. Moja kwa moja nikawaza, "Naamini nitaona kama atasema kama hao wengine." Nikageuka, nikafikiri, "Loo, jamani! Hiyo ingenitetemesha, najua." Maana, nilichukia kuwazia jambo hilo. Nikageuka.

¹⁷³ Akasema, "Pengine yanipasa nijieleze." Akasema, "Mimi ni mnajimu."

Nikasema, "Nilifikiria ulikuwa kitu kama hicho."

¹⁷⁴ Akasema, "Niko njiani kuelekea Chicago kumwona mvulana wangu ambaye ni mhudumu wa Kibaptisti."

Nikasema, "Ndiyo, mama."

¹⁷⁵ Akasema, "Mtu yeyote amewahi kukwambia ulizaliwa chini ya ishara?"

¹⁷⁶ Nikasema, "La, mama." Nilimdanganya hapo, unaona, na nikasema... nilitaka tu nione vile alikuwa anaenda kusema. Ndipo akasema... nikasema, "La, mama."

Basi akasema, "Hivi si... Wahudumu hawajawahi kukwambia?"

Nikasema, "Sina uhusiano wowote na wahudumu."

Naye akasema, "A-ha."

Ndipo nikasema... a—akaniambia... Nikasema, "Vema..."

¹⁷⁷ Akasema, "Kama nikikwambia ni lini hasa ulipozaliwa, je! utaniamini?"

Nikasema, "La, mama."

Basi akasema, "Vema, ninaweza kukwambia ulizaliwa lini."

Nikasema, "Siamini hilo."

¹⁷⁸ Naye akasema, "Ulizaliwa tarehe 6 Aprili, 1909, saa kumi na moja asubuhi."

¹⁷⁹ Nikasema, "Hiyo ni kweli." Nikasema, "Unajuaje hilo?" Nikasema, "Mwambie huyu baharia hapa alizaliwa lini."

Kasema, "Siwezi."

Nami nikasema, "Kwa nini? Unajuaje?"

¹⁸⁰ Kasema, "Angalia, bwana." Akasema, alipoanza kuzungumza juu ya elimu hii ya nyota sasa, naye akasema, "Kila baada ya miaka kadhaa..." Kasema, "Unakumbuka wakati ile nyota ya asubuhi ilipokuja, ile iliyowaongoza mamajusi kwa Yesu Kristo?"

¹⁸¹ Nami kwa namna fulani nikasita, mwajua, nikasema, "Vema, sijui chochote kuhusu dini."

¹⁸² Naye akasema, “Vema, umesikia kuhusu mamajusi wakija kumwona Yesu.”

Nikasema, “Ndiyo.”

Naye akasema, “Vema, mamajusi walikuwa nini?”

“Loo,” nikasema, “walikuwa ni mamajusi tu, nijuavyo mimi.”

¹⁸³ Akasema, “Vema, mamajusi ni mtu gani?” Akasema, “Kitu kile kile nilicho mimi, mtaalamu wa nyota, ‘mchunguza nyota’ ndivyo wanavyowaita.” Kisha akasema, “Unajua, kabla ya Mungu kufanya kitu chochote du—duniani, Yeye daima hukitangaza kule mbinguni, na kisha duniani.”

Nami nikasema, “Sijui.”

¹⁸⁴ Basi akasema, “Vema . . .” Akataja mbili au tatu, mbili . . . nyota tatu, kama Mirihi, Jupita, na Zuhura. Hazikuwa ndizo, bali alisema, “Zilivuka njia zao zikakutana na kufanya . . .” Kasema, “Kulikuwa na mamajusi watatu waliokuja kukutana na Bwana Yesu, na mmoja alitoka katika ukoo wa Hamu, na mmoja Shemu, na mwingine Yafethi.” Kisha kasema, “Walipokutana pamoja kule Bethlehemu, nyota zile tatu ambako walitoka . . . Kila mtu duniani,” kasema, “wana uhusiano fulani na nyota.” Kasema, “Muulize huyo baharia hapo wakati mwezi uwapo kiza na sayari ya mbingu inapoondoka, maji kujaa na kupwa hakuendi pamoja nayo na kurudi pamoja nayo.”

Nikasema, “Sina haja nimuulize hilo, ninajua hilo.”

¹⁸⁵ Basi akasema, “Vema, kuzaliwa kwako kuna uhusiano fulani na nyota kule juu.”

Nami nikasema, “Vema, hilo mimi sijui.”

¹⁸⁶ Kisha akasema, “Sasa, hawa mamajusi watatu walikuja.” Ndipo kasema, “Wakati hizo nyota tatu, wakati hizo . . . Zilitokea pande tofauti zikakutana Bethlehemu. Nao walisema waliona na kushauriana, na mmoja alitoka katika ukoo wa Hamu, Shemu, na Yafethi, wale wana watatu wa Nuhu.” Naye akasema, “Kisha wakaja wakamwabudu Bwana Yesu Kristo.” Na akasema “Walipoondoka,” kasema, “walileta tunu na kumpa Yeye.”

¹⁸⁷ Ndipo kasema, “Yesu Kristo alisema katika huduma Yake ya kwamba wakati Injili hii itakapokuwa imehubiriwa ulimwengu mzima (watu wa Hamu, Shemu na wa Yafethi), basi atakuja tena.” Kisha akasema, “Sasa, hizo sayari, sayari za mbinguni, zinapozunguka . . .” Kasema, “Zilitengana. Hazijakuwa duniani tangu wakati huo, ijulikanavyo. Lakini” kasema “kila muda wa mamia kadhaa ya miaka, hukungama mizunguko yao namna *hii*.” Kama ikitokea kwamba kuna mwenye elimu ya nyota hapa, unaweza kujua kile alichokuwa akizungumzia. Mimi sijui. Kwa hiyo alipokuwa anazu- . . . Kasema, “Hupitana namna hiyo.” Kisha kasema, “Kwa ukumbusho wa Kipawa kikuu kuliko vyote wanadamu walichowahi kupewa, hapo Mungu alipomtoa

Mwana Wake. Wakati sayari hizi zipitanapo tena, mbona," kasema, "Yeye hutuma kipawa kingine duniani." Basi kasema, "Wewe ulizaliwa kwenye kuingamana kwa wakati huo." Halafu kasema, "Hiyo ndiyo sababu nilijua hilo."

¹⁸⁸ Vema, basi nikasema, "Mama, jambo la kwanza, siamini chochote kuhusu hayo. Mimi si wa kidini, na sitaki kusikia tena kuhusu jambo hilo!" Nikaondoka. Na kwa hiyo nikamkatiza mara moja vizuri sana. Kwa hiyo nikatoka nikaenda.

¹⁸⁹ Na kila wakati yeyote . . . ninapokuwa karibu na mmoja wao, hivyo ndivyo mambo yangekuwa. Nami nikawaza, "Kwa nini hao pepo wanafanya hivyo?"

¹⁹⁰ Halafu wahubiri, wakisema, "Huyo ni ibilisi! Huyo ni ibilisi!" Walinifanya niliamini.

¹⁹¹ Na basi usiku ule huko juu wakati mimi . . . wakati Yeye aliporejea kwenye jambo hilo, nilimuuliza, nikasema, "Vema, hivi ni kwa nini hao wanaowasiliana na mizimu wote na vitu vya namna hiyo, na hao watu waliopagawa na pepo, iwe sikuzote wananiambia kuhusu jambo Hilo; na makasisi ambao, ndugu zangu, wananiambia ya kwamba ni cha roho mwovu?"

¹⁹² Sasa hebu sikilizeni aliyosema Yeye, Huyu Ambaye ananing'inia juu kule kwenye ile picha. Alisema, "Kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo na sasa." Naye akaanza kunitajia, ya kwamba, "Wakati huduma ya Bwana wetu Yesu Kristo ilipoanza kutenda kazi, wahudumu walisema, 'Yeye alikuwa ni Beelzebuli, ibilisi'; lakini pepo wakasema, 'Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, Mtakatifu wa Israeli.' Pepo . . . Basi mwangalie Paulo na Barnaba walipokuwa kule juu wakihubiri. Wahudumu walisema, 'Watu hawa wanaupindua ulimwengu juu chini. Ni wabaya, ni—ni ibilisi.' Na maskini kizee mpiga ramli huko barabarani, alitambua ya kwamba Paulo na Barnaba walikuwa watu wa Mungu, kasema, 'Ni watu wa Mungu wenye kutuambia njia ya Uzima.'" Je! hiyo ni kweli? "Wenye kuwasiliana na mizimu na watabiri, watu waliopagawa na pepo."

¹⁹³ Bali sisi tunaharibiwa sana na theolojia mpaka hatujui chochote kuhusu Roho. Natumaini mtanipenda baada ya hapa. Bali hivyo ndivyo ilivyo. Namaanisha Pentekoste, pia! Hiyo ni kweli. Kupiga makelele tu na kucheza cheza huku na huko hakumaanishi unajua chochote kuhusu Roho.

¹⁹⁴ Ni uhusiano wa kibinafsi, ana kwa ana, hicho ndicho unachohitaji. Hilo ndilo aina ya Kanisa Mungu analotaka kuinuia, hiyo ni kweli, wanapokutanika pamoja katika umoja na nguvu, katika Roho.

¹⁹⁵ Naye alirejea kwenye jambo hilo. Naye akaniambia jinsi ambavyo kwamba huduma ilielewa Hilo vibaya, na akanihakikishia kwamba huduma ilikuwa imelielewa Hilo

vibaya. Na wakati Yeye aliponiambia yote kuhusu jambo hili na jinsi kwamba Yesu. . .

¹⁹⁶ Nikasema, “Vema, vipi kuhusu hili, mambo haya ambayo yananifanyikia?”

¹⁹⁷ Na, unaona, Yeye akasema, “Hayo yataongezeka na kuwa makubwa zaidi na zaidi.” Naye akanitajia, akiniambia jinsi Yesu alivyofanya hayo; jinsi ambavyo Yeye alikuja na akajawa na Nguvu ambayo iliweza kujua mambo kabla na kuwaambia wale wanawake kisimani, hakudai kuwa mponya, akadai kutenda mambo yale vile tu Baba alivyomwonyesha.

Nikasema, “Vema, hiyo ingekuwa ni roho ya aina gani?”

Akasema, “Ilikuwa ni Roho Mtakatifu.”

¹⁹⁸ Ndipo kitu fulani pale kikatukia ndani yangu, hata nikatambua kwamba kitu kile hasa nilichokipa kisogo ndicho ambacho Mungu alinileta hapa kwa ajili yake. Kisha nikatambua ya kwamba ilikuwa tu ni kama wale Mafarisayo katika siku zilizopita, walikuwa wamenifasiria vibaya Maandiko. Kwa hiyo tangu wakati huo na kuendelea nilichukua tafsiri yangu mwenyewe ya jambo Hilo, yale Roho Mtakatifu aliyosema.

Nikamwambia, “Ningekwenda.”

Akasema, “Nitakuwa pamoja nawe.”

¹⁹⁹ Naye yule Malaika akaingia kwenye Nuru tena ambayo ilianza kuzunguka na kuzunguka, na kuzunguka na kuzunguka, na kuzunguka penye miguu Yake namna hiyo, akaenda juu katika ile Nuru na akatoka katika lile jengo.

Nikaenda nyumbani nikiwa mtu mpya.

²⁰⁰ Nikaenda kanisani na kuwaambia watu kuhusu jambo hilo. Ile. . . ilikuwa Jumapili usiku.

²⁰¹ Na usiku wa Jumatano walimleta mwanamke pale, mmoja wa manesi wa Mayo akifa kwa kansa, amebakia kivuli tu. Niliposhuka nikaenda ili nimshike, likatokea ono mbele yake, likamwonyesha akiwa amerejea kwenye unesi tena. Naye yuko kwenye orodha huko Louisville, “amekufa kwa miaka mingi.” Yuko huko Jeffersonville sasa, anafanya kazi ya unesi, amekuwa akifanya unesi kwa miaka mingi. Kwa kuwa, niliangalia juu kule, na nikaona lile ono. Nikageuka, hata sikujua lile nililokuwa nikifanya, nikiwa nimesimama pale, nilitetemeka hapo mara ya kwanza walipomleta mgonjwa huyo na kumlaza pale chini. Na manesi na kadhalika wakisimama kumzunguka, naye amelala hapo, na uso wake wote umedidimia ndani na macho yake tayari yamepinduka.

²⁰² Margie Morgan. Kama unataka kumwandikia, ni 411 Knobloch Avenue, Jeffersonville, Indiana. Ama uandikie Clark

County Hospital, Jeffersonville, Indiana. Mwacheni awape huo—huo ushuhuda.

203 Nikatazama chini kule. Na mgonjwa huyo wa kwanza pale, kuona hapa anatokea, ono likatokea. Nili mwona mwanamke huyo akifanya unesi tena, akienda huku na huko, ni mzima na mwenye nguvu na afya. Nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Utaishi wala hutakufa!’”

204 Mume wake, mtu wa juu sana katika mambo ya ulimwengu huu, aliniangalia namna *hiyo*. Nikasema, “Bwana, usiogope! Mkeo ataishi.”

205 Akaniita nje, kasema... akawaita madaktari wawili au watatu, kasema, “Unawajua?”

Nikasema, “Ndiyo.”

206 “Mbona,” kasema, “nimecheza gofu na yeye. Akasema, ‘Hiyo kansa ilikuwa imezunguka utumbo wake, huwezi kumsafisha hata kwa enema.’”

207 Nikasema, “Sijali ana nini! Kitu fulani ndani hapa, niliona ono! Na Mtu yule aliyeniambia, kasema, chochote nilichooni, nikiseme na kingekuwa hivyo. Naye aliniambia nami ninaliamini.”

208 Mungu asifiwe! Siku chache kuanzia hapo alikuwa anafua, akienda huku na huko. Ana uzito wa kama ratili mia moja sitini na tano sasa, akiwa mwenye afya kamili.

209 Basi nilipokikubali, kikaanza kuenea. Ndipo Robert Daugherty akanipigia simu. Na hapa kikaenda, kupitia chini huko Texas, kote ulimwenguni.

210 Ndipo usiku mmoja, kwenye yapata mara nne au tano huko nje... Nisingeweza kuelewa kunena kwa lugha na kadhalika. Niliamini ubatizo wa Roho Mtakatifu, nikaamini watu wangeweza kunena kwa lugha. Na usiku mmoja wakati nilipokuwa nikitembea huko kuelekea kule... katika kanisa kuu la dayosisi, San Antonio, Texas, nikiwa ninatembea huko, maskini jamaa fulani aliyeketi hapa juu akaanza kunena kwa lugha kama bunduki ya marisaa ikifyatua risasi, ama bombom, ikipiga mfululizo. Upande wa nyuma, nyuma kabisa huko, jamaa fulani aliinuka na akasema, “BWANA ASEMA HIVI! Mtu huyu anayekwenda jukwaani anaenenda akiwa na huduma ambayo imeamriwa na Mwenyezi Mungu. Na kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kama mtangulizi wa kwanza wa kuja kwa Yesu Kristo, vivyo hivyo amebeba Ujumbe ambao utaanzisha Kuja kwa Pili kwa Bwana Yesu Kristo.”

211 Karibu nididimie kwenye viatu vyangu. Nikainua macho yangu, nikasema, “Unamjua mtu huyo?”

Akasema, “La, bwana.”

Nikasema, “Unamjua?”

Akasema, “La, bwana.”

Nikasema, “Unanijua mimi?”

Akasema, “La, bwana.”

Nikasema, “Unafanya nini hapa?”

212 Akasema, “Nililisoma kwenye gazeti.” Na kwa kawaida . . . Huo ulikuwa ndio usiku wa kwanza wa mkutano.

Nikatazama kule na nikasema, “Ulikujaje hapa?”

213 Kasema, “Baadhi ya watu wangu waliniambia kwamba utakuwepo hapa, ‘mponyaji wa Kiungu,’ ndipo nikaja.”

Nikasema, “Hivi nyinyi nyote hamfahamiani?”

Akasema, “La.”

214 Loo, jamani! Hapo nikaona kwamba nguvu zenyewe za Roho Mtakatifu . . . Ambapo wakati mmoja huko nyuma nilikuwa nimefikiria lilikuwa ni kosa, na nikajua ya kwamba mimi . . . Malaika yuyu wa Mungu alihusishwa na watu hao waliokuwa na vitu hivyo. Ijapokuwa walikuwa na mambo bandia na michanganyiko mingi na kuboboja kwingi ndani yake, lakini humo ndani kulikuwa na kitu halisi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Kristo. Na niliona kwamba ili—ilikuwa kweli.

215 Loo, miaka mingi ikapita, na katika mikutano watu wangeona, maono na kadhalika.

216 Wakati mmoja mpiga picha mmoja aliipiga Hiyo picha nilipokuwa nimesimama mahali fulani chini huko Arkansas, naamini ilikuwa huko, kwenye mkutano kama huu, ukumbi wa mikutano kama huu. Nami nilikuwa nimesimama, nikijaribu kuielezea Hiyo. Watu walijua, wangeketi na kusikiliza, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, na kadhalika. Na halafu ikawa nikatazama, ikiingia mlangoni, Hii hapa ikaja, ikifanya, “Whoossh, whoossh!”

217 Nikasema, “Haitanilazimu kuzungumza tena, kwani Hii hapa inakuja sasa.” Nayo ikapanda, na watu wakaanza kupiga mayowe. Ikaja pale nilipokuwa na kutulia pale.

218 Wakati ilipokuwa tu inatulia, mhudumu mmoja akaja mbio akasema, “Aisee, ninaiona Hiyo!” Nayo ikampiga akawa kipofu kama—kama alivyoweza kuwa, akarudi nyuma akipepesuka. Unaweza kuangalia picha yake moja kwa moja pale kwenye kitabu na uone hilo wakati alipopepesuka akirudi nyuma huku ameinamisha kichwa chake chini namna hiyo. Waweza kuona picha yake.

219 Na hapo ikatulia. Ni mpiga picha wa magazeti tu aliyeipiga picha wakati huo. Lakini Bwana hakuwa tayari.

220 Basi usiku mmoja huko Houston, Texas, wakati, loo, maelfu mara maelfu ya watu . . . Tulikuwa na mia nane . . . elfu nane huko kwenye kile mnachokiita, huko kwenye ukumbi wa muziki,

kurudi tena kwenye Ukumbi mkuu wa Maonyesho wa Sam Houston.

221 Na hapo katika mjadala ule usiku huo, wakati mhubiri mmoja wa Kibaptisti aliposema mimi “sikuwa chochote ila mnafiki duni sana na laghai, laghai wa kidini, na anayepaswa kufukuzwa kutoka mjini” na yeye ndiye anayepaswa kutenda jambo hilo.

222 Ndugu Bosworth akasema, “Ndugu Branham, utaachilia kitu kama hicho kitendeke? Mwrite mshindane!”

223 Nikasema, “La, bwana, siamini katika kuzozana. Injili haikufanywa kwa kusudi la kuzozana, imefanywa kwa kusudi la kuishi.” Kisha nikasema, “Hata ungemshawishi jinsi gani, ataendelea na mwelekeo uo huo tu.” Nikasema, “Yeye... haingemfanya yeye tofauti hata kidogo. Kama Mungu hawezi kuzungumza na moyo wake, mimi ninawezaje?”

224 Siku iliyofuatia ikatokea, akasema, “Inaonyesha wana kitu gani ndani yao,” Houston Chronicle. Lasema, “Inaonyesha wana kitu gani ndani yao, wanaogopa kutetea yale wanayoyahubiri.”

225 Mzee Ndugu Bosworth alinijia, akiwa amesonga mbele kwenye miaka yake ya sabini wakati huo, ndugu mpendwa mzee, akanikumbatia kwa mkono wake, kasema, “Ndugu Branham,” akasema, “unamaanisha hutalishughulikia jambo hilo?”

226 Nikasema, “La, Ndugu Bosworth. La, bwana. Sitalishughulikia.” Nikasema, “Halifai kitu.” Nikasema, “Inasababisha tu kuzozana tunapoondoka jukwaani.” Nikasema, “Ninafanya mkutano sasa, nami sitaki kufanya mambo yavurugike namna hiyo.” Nikasema, “Mwache tu aendele.” Nikasema, “Ni hayo tu, yeye anapayuka tu.” Nikasema, “Tumekuwa na hao hapo kabla, na haifai kitu kuzungumza nao.” Nikasema, “Wataondoka moja kwa moja, wakijishikilia.” Nikasema, “Kama wakiwahi kupokea ujuzi wa ile Kweli na kisha wasiipokee Hiyo, Biblia ilisema wamevuka mstari wa kutenganisha na hawatasamehewa kamwe katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao. Wanaiita Hiyo ‘ibilisi’ na hawawezi kujizuia. Wamepagawa na roho wa kidini ambaye ni ibilisi.”

227 Ni wangapi wanajua hiyo ni kweli, ya kwamba roho wa ibilisi ni wa kidini? Naam, bwana, ni wa kimsingi tu kama wawezavyo kuwa. Na kwa hiyo, basi, hilo halikukolea vizuri sana niliposema “kimsingi,” bali hiyo ni kweli. “Wakiwa na mfano wa utauwa na kukana Nguvu zake.” Hiyo ni kweli. Ishara na maaajabu ndiyo yanayomthibitisha Mungu, daima. Na Yeye alisema itakuwa katika siku za mwisho jambo lile lile. Basi angalia!

228 Mzee Ndugu Bosworth, mimi... alikuwa aje pamoja nami, naye alikuwa kidogo amechoka. Amerudi tu kutoka Japani. Alikuwa anaenda kuwepo hapa. Atakuwepo huko Lubbock

pamoja nami. Na kwa hiyo alikuwa...alikuwa na, maskini mafua makali, hivyo hakuweza kuja kwenye huu, yeye na mke wake. Na kwa hiyo yeye...

²²⁹ Wote walifikiri anafanana na Kaleb. Alisimama pale, akasema, “Vema, Ndugu Branham,” ule mtazamo wa heshima kabisa, mwajua, akasema, “niruhusu niende nikalishughulikie,” kisha akasema “iwapo wewe hutaki kulishughulikia.”

²³⁰ Nikasema, “Ee Ndugu Bosworth, si—sitaki wewe ulishughulikie. Utaanza kuzozana.”

Akasema, “Hakutakuwa na neno hata moja la kuzozana.”

²³¹ Sasa, kabla tu sijafunga, sikilizeni hili. Alishuka akaenda huko chini. Nikasema, “Kama hamtazozana, sawa.”

Kasema, “Ninaahidi kutokuzozana.”

²³² Watu kama thelathini elfu walikusanyika kwa ajili ya ukumbi huo wa mikutano usiku huo. Ndugu Wood, anayeketi hapa, alikuwapo wakati huo, na alikuwa ameketi katika ukumbi huo. Nami...

²³³ Mvulana wangu akasema, au...Mke wangu akasema, “Hushuki kwenda huko kwenye huo mkutano?”

²³⁴ Nikasema, “La. Nisingeenda huko na kuwasikia wakizozana. La, bwana. Nisingeshuka kwenda chini huko na kusikiliza hilo.”

Wakati wa usiku ulipoingia, Kitu fulani kikasema, “Shuka uende huko chini.”

²³⁵ Nikachukua teksa, ndugu yangu, na mke na watoto wangu, tukashuka tukaenda. Nami nilikuwa nimepanda juu kwenye roshani ya thelathini, juu sana namna hiyo, nikaketi.

²³⁶ Mzee Ndugu Bosworth akatoka pale akitembea kama maskini mwanadiplomasia, wajua. Alikuwa amenakili baadhi ya...Alikuwa na ahadi mia sita mbalimbali za Biblia zilizopakiliwa kule. Akasema, “Sasa, Daktari Best, naomba upande juu hapa uchukue moja ya ahadi hizi na kuikanusha kwa Biblia. Kila moja ya ahadi hizi iko katika Biblia, zinazomhusu Yesu Kristo kuwaponya wagonjwa katika siku hii. Kama unaweza kuchukua mojawapo ya ahadi hizi na, kwa Biblia, uikanushe kwa Biblia, nitaketi chini, nikupe mkono, niseme, ‘Uko sahihi.’”

²³⁷ Akasema, “Nitalishughulikia hilo nitakapopanda hapo juu!” Alitaka awe wa mwisho kusudi aweze kuyafutilia mbali aliyosema Ndugu Bosworth, unaona.

²³⁸ Basi Ndugu Bosworth akasema, “Vema, Ndugu Best, nitakuuliza moja, na kama utanijibu ‘ndiyo’ ama ‘la,’” kasema, “tutaumaliza tu huu mjadala sasa hivi.”

Naye akasema—akasema, “Nitashughulikia hilo!”

Akamuuliza yule mwamuzi kama angeweza kumuuliza. Kasema, “Ndiyo.”

²³⁹ Akasema, “Ndugu Best, je! majina ya ukombozi ya Yehova yalitumiwa kwa Yesu? ‘Ndiyo’ au ‘la’?”

²⁴⁰ Hilo lilimaliza kila kitu. Hakukuwa na lingine. Nakwambia, nilihisi tu kitu fulani kikipitia tu kila mahali ndani yangu. Sikuwahi kuwazia hilo, mimi mwenyewe, unaona. Ndipo nikawaza, “Loo, jamani, hawezi kujibu! Hilo linafunga jambo hilo.”

Akasema, “Vema, Daktari Best, mimi—mimi nina hofu.”

Akasema, “Nitalishughulikia hilo!”

²⁴¹ Kasema, “Nahofia kwamba huwezi kujibu swali langu lililo rahisi kuliko yote.” Alikuwa ametulia tu kama tango, naye alijua mahali alipokuwa amesimama. Kwa hiyo basi aliketi tu pale akiwa na Andiko lile.

Kasema, “Chukua dakika zako thelathini, nitajibu baada ya hizo!”

²⁴² Ndipo mzee Ndugu Bosworth akaketi pale na kuchukua Maandiko hayo na kumfunga mtu huyo kufikia mahali ambapo uso wake ulikuwa mwekundu sana hata karibu, ungeweza kuwasha njiti ya kiberiti juu yake.

²⁴³ Akainuka kutoka hapo, mwenye hasira, akayatupa makaratasi kote sakafuni, akaenda juu pale na kuhubiri ujumbe mzuri wa Kikampbeli. Mimi nilikuwa Mbaptisti, najua kile wanachoamini. Yeye kamwe... Alikuwa anahubiri juu ya ufufuo, “‘wakati huu upatikanao na mauti utakapovaa kutopatikana na mauti,’ ndipo tutakapokuwa na uponyaji wa Kiungu.” Loo, jamani! Tuna haja gani na kuponya Kiungu baada sisi kuwa wasiopatikana na mauti (“wakati huu upatikanao na mauti utakapovaa kutokupatikana na mauti,” ufufuo wa wafu)? Hata alishuku mwujiza ambao Yesu aliufanya kwa Lazaro, kasema, “Alikufa tena, na hicho kilikuwa ni kitu cha muda tu.” Mnaona?

²⁴⁴ Naye alipomaliza namna hiyo, alisema, “Mleteni huyo mponyaji wa Kiungu nimwone akitenda!”

²⁴⁵ Wakawa na kusitasita kidogo hapo. Ndugu Bosworth akasema, “Mimi nimeshangazwa na wewe, Ndugu Best, kwa kutojibu hata swali moja nililokuuliza.”

²⁴⁶ Na kwa hiyo hapo akachemka kwelikweli, akasema, “Mleteni huyo mponyaji wa Kiungu na hebu nimwone akifanya!”

Kasema, “Ndugu Best, unaamini katika kuokolewa kwa watu?”

Akasema, “Hakika!”

Akasema, “Je! wewe ungetaka kuitwa mwokozi wa Kiungu?”

Kasema, “Bila shaka hapana!”

247 “Wala... Hilo halingekufanya mwokozi wa Kiungu kwa sababu ulihubiri wokovu wa nafsi.”

Akasema, “Vema, bila shaka hapana!”

248 Kasema, “Wala hilo halimfanyi Ndugu Branham mponyaji wa Kiungu kwa kuhubiri kuponya Kiungu kwa ajili ya mwili. Yeye si mponyaji wa Kiungu, yeye huwaelekeza watu kwa Yesu Kristo.”

249 Naye akasema, “Mleteni, hebu nimwone akifanya! Ngojeni niwaangalie hao watu, mwaka mmoja tangu leo, nami nitawaambia kama nitaamini Hilo au la.”

250 Ndugu Bosworth akasema, “Ndugu Best, hilo linasikika kama kisa kingine cha pale Kalvari, ‘Shuka Msalabani nasi tutakuamini.’” Mnaona?

251 Na kwa hiyo, loo, ndipo akafoka kwelikweli. Akasema, “Hebu nimwone akifanya! Hebu nimwone akifanya!” Wale waamuzi wakamketisha chini. Akaenda kule, na kulikuwa na mhubiri wa Kipentekoste amesimama pale, akamzaba tu kofi kote kupitia jukwaani. Na kwa hiyo wakamkomesha wakati huo. (Basi Ndugu Bosworth akasema, “Hapa, hapa!, La, la.”) Kwa hiyo wale waamuzi wakamfanya kuketi chini.

252 Raymond Richey akasimama, kasema, “Hivi huu ndio msimamo wa Shirika la Wabaptisti wa Kusini?” Kasema, “Ninyi wahudumu wa Kibatisti, je! Shirika la Wabatisti wa Kusini ndilo lililomtuma mtu huyu hapa ama alikuja mwenyewe?” Hawangejibu. Akasema, “Nimewauliza!” Aliwajua, kila mmoja.

253 Wakasema, “Alikuja mwenyewe.” Kwa sababu ninajua Wabaptisti wanaamini katika uponyaji wa Kiungu, pia. Kwa hiyo basi akasema, “Alikuja mwenyewe.”

254 Kwa hiyo basi hili ndilo lililotukia wakati huo. Ndipo Ndugu Bosworth akasema, “Ninajua Ndugu Branham yupo mkutanoni, kama akitaka kuja na kuruhusu wasikilizaji kuondoka, vyema sana.”

Basi Howard akasema, “Wewe kaa kimya!”

Nikasema, “Mimi ninakaa kimya.”

255 Na papo hapo Kitu kikaja pale, kikaanza kuzungukazunguka, nami nilijua ilikuwa ni Malaika wa Bwana, kasema, “Amka!”

256 Yapata watu mia tano waliweka mikono yao pamoja namna *hii*, wakafanya mstari, kuja mpaka jukwaani.

257 Nikasema, “Marafiki, mimi si mponyaji wa Kiungu. Mimi ni ndugu yenu.” Nikasema, “Ndugu Best, bila ya...” Au, “Ndugu Best,” nikasema, “bila ya kukudharau, ndugu yangu,

hata kidogo. Wewe unayo haki kuamini unayoamini binafsi, na mimi pia.” Nikasema, “Bila shaka, unaona hukuweza kamwe kuthibitisha hilo, hoja yako, kwa Ndugu Bosworth. Wala usingeweza kwa mtu yeyote yule ambaye amefunzwa vyema katika Biblia, anayeyajua mambo hayo.” Nikasema, “Na kuhusu kuwaponya watu, siwezi kuwaponya, Ndugu Best. Lakini mimi nipo hapa kila usiku, kama unataka kumwona Bwana akitenda miujiza, njoo. Yeye hutenda hilo kila usiku.”

²⁵⁸ Na akasema, “Ningependa kukuona ukimponya mtu fulani na uniache niwachunguze! Unaweza uwapumbaze akili kwa ujanja wako, bali,” kasema “ningetaka kuona jambo hilo mwaka mmoja tangu hapo!”

Nikasema, “Vema, ungekuwa na haki ya kuwachunguza, Ndugu Best.”

²⁵⁹ Akasema, “Hakuna chochote isipokuwa nyinyi kundi la baradhuli watakatifu wanaojibingirisha mnaoamini takataka kama hiyo. Wabaptisti hawaamini upuuzi kama huo.”

²⁶⁰ Ndugu Bosworth akasema, “Hebu kidogo.” Kasema, “Ni watu wangapi huko nje, katika majuma haya mawili ya mkutano hapa, ambao wana msimamo mzuri na haya makanisa mazuri ya Kibaptisti hapa Houston, ambao mnaweza kuthibitisha kwamba mmeponywa na Mwenyezi Mungu wakati Ndugu Branham amekuwepo hapa?” Na zaidi ya mia tatu wakasimama. Kasema, “Vipi kuhusu hilo?”

²⁶¹ Akasema, “Hao si Wabaptisti!” Kasema, “Mtu yeyote anaweza kushuhudia chochote, hiyo bado haifanyi hicho kuwa sahihi!”

²⁶² Kasema, “Neno la Mungu linasema ni sahihi, nawe huwezi kupingana na jambo hilo. Na hao watu wanasema ni sahihi, na huwezi kukanusha jambo hilo. Kwa hiyo mtafanya nini kuhusu jambo Hilo?” Mnaona, namna hiyo.

²⁶³ Nikasema, “Ndugu Best, mimi husema tu iliyo Kweli. Na kama mimi ni mkweli, Mungu anawajibika kuunga mkono Kweli hiyo.” Nikasema, “Kama haliungi mkono... Kama Yeye hataunga mkono hiyo Kweli, basi Yeye si Mungu.” Nami nikasema, “Mimi siponyi watu. Nilizaliwa na—na karama kuona vitu, kuviona vikitendeka.” Nikasema, “Najua mimi ninaeleweka vibaya, bali siwezi kufanya zaidi ya kutimiza ninachosadiki moyoni mwangu.” Nikasema, “Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo alifufuka kutoka kwa wafu. Na kama yule Roho anayekuja na kuonyesha maono na kadhalika, kama hilo linaleta swali, fika hapa uone.” Nikasema, “Ni hayo tu.” Lakini nikasema, “Lakini kwangu mimi, siwezi kufanya lolote kwa nafsi yangu.” Kisha nikasema, “Kama nikisema kweli, Mungu anao wajibu kwangu, kushuhudia ya kwamba Hilo ni Kweli.”

²⁶⁴ Na mnamo wakati huo, Kitu fulani kikafanya, “Whooooosssh!” Hapa akaja, akishuka moja kwa moja. Na

Shirika la Wapiga Picha wa Marekani, Studio za Douglas huko Houston, Texas, wakiwa na kamera kubwa imewekwa pale (huwa wanakatazwa kupiga picha), wakapiga picha.

²⁶⁵ Wakati walipokuwa pale kwa ajili ya kumpiga picha Bw. Best, ndipo a—akasema, kabla sijashuka kwenda kule, akasema, “Ngoja kidogo! Nina picha sita zinazokuja hapa!” Akasema, “Hapa, nipige picha sasa!” Ndipo akakitia kidole chake kwenye pua ya yule mzee mtauwa, namna hiyo, kasema, “Sasa nipige picha!” Nao wakampiga. Halafu akanyosha ngumi yake akaiinua juu, kasema, “Sasa nipige picha!” Nao wakapiga namna hiyo. Halafu akafanya namna hiyo, kusimama apigwe picha. Akasema, “Mtaona hii kwenye jarida langu!” namna hiyo.

²⁶⁶ Ndugu Bosworth alisimama pale na hakusema chochote. Halafu wakapiga tu picha ya Hii.

²⁶⁷ Akiwa njiani kwenda zake nyumbani usiku huo, (mvulana wa Katoliki ndiye aliyepiga picha hiyo), alimwambia huyu mvulana mwingine, akasema, “Wasemaje juu ya Hiyo?”

²⁶⁸ Akasema, “Mimi najua nilimkosoa. Ile tezi iliyotoweka kwenye koo la yule mwanamke, nilisema alimpumbaza akili.” Kasema, “Huenda nilikosea juu ya hilo.”

Kasema, “Wasemaje juu ya ile picha?”

“Sijui.”

²⁶⁹ Wakaiweka kwenye asidi. Hii hapa picha yake, waweza kumuuliza ukitaka. Wakaenda nyumbani, akaketi hapo na kuvuta sigara. Akaingia ndani akachomoa moja ya Ndugu Bosworth, ilikuwa negativu. Akachomoa mbili, tatu, nne, tano, sita, na kila moja ya hizo ilikuwa tupu. Mungu asingeruhusu picha ya mzee Wake mtauwa akiwa amesimama pale pamoja na yule mnafiki, na pua yake, ama mkono, ngumi ikitikiswa chini ya pua yake namna hiyo. Asingeliruhusu hilo.

²⁷⁰ Wakachomoa ile nyingine, na Hii hapa. Huyu mtu alipatwa na mshtuko wa moyo, walisema, usiku huo.

²⁷¹ Na wakatuma hii negativu huko Washington, DC. Ikapewa hakinakili, ikarudishwa.

²⁷² Naye George J. Lacy, mkuu wa F.B.I. katika alama za vidole na hati, na kadhalika, mmoja wa walio mashuhuri sana katika ulimwengu mzima, aliletwa kule na akawekwa siku mbili kwenye hiyo kuichunguza ile kamera, taa, kila kitu kingine. Basi tulipokuja alasiri ile, akasema, “Kasisi Branham, mimi nimekuwa mkosowaji wako, pia.” Akasema, “Nami nilisema ilikuwa ni saikolojia, mtu fulani alisema walikuwa wameziona hizo Nuru na mambo kama hayo.” Kisha kasema, “Unajua, yule mnafiki wa kale alikuwa akisema hayo” (alimaanisha asiyeamini) “hizo picha zilizomzunguka, hiyo duara ya nuru iliyomzunguka Kristo, inayowazunguka

watakatifu,' akasema, 'hiyo ilikuwa tu ni saikolojia.'" Lakini kasema, "Kasisi Branham, jicho la mtambo wa kamera hii halipigi saikolojia picha! Nuru iligonga lenzi, ama iliigusa ile negativu, na ilikuwa hapo." Kisha akasema. . .

²⁷³ Nikaikabidhi kwao. Akasema, "Loo, bwana, unajua thamani ya hiyo?"

Nami nikasema, "Si kwangu mimi, ndugu, si kwangu mimi." Basi kwa hiyo akasema. . .

²⁷⁴ "Kwa kweli, haitatambulikana wakati ungali hai, lakini siku moja, kama ustaarabu ukiendelea na Ukristo ukidumu, kutakuwa na jambo litakalotukia kuihusu hii."

²⁷⁵ Kwa hiyo, marafiki, usiku wa leo, kama huu ndio mkutano wetu wa mwisho humu duniani, mimi na wewe tumeketi katika Uwepo wa Mwenyezi Mungu. Ushuhuda wangu ni kweli. Mambo mengi, mengi sana, ingechukua vitabu chungu nzima kuliandika jambo hilo, bali nawatakeni ninyi mjue.

²⁷⁶ Ni wangapi hapa ndani ambao hasa, bila ya hiyo picha, wameona Nuru hiyo Yenyewe ikisimama kuzunguka mahali nilipokuwa ninahubiri? Inueni mikono yenu, kote katika jengo, yeyote aliyewahi kuiona Hiyo. Mnaona, yapata mikono kama minane au kumi ya walioketi hapa.

²⁷⁷ Unasema, "Wangeweza—wangeweza kuiona na mimi nisiione?" Naam, bwana.

²⁷⁸ Ile—ile Nyota ambayo wale mamajusi walikuwa wakiifuata, ilipita juu ya kila kituo cha uchunguzi wa anga. Hakuna mtu aliyeiona Hiyo ila wao. Hao tu ndio walioiona Hiyo.

²⁷⁹ Eliya alikuwa amesimama pale akiangalia magari yale yote ya moto, na kila kitu kingine. Naye Gehazi aliangalia huku na huko, hakuweza kuwaona popote. Mungu akasema, "Mfungue macho apate kuona." Na ndipo akayaona, unaona. Lakini alikuwa ni mvulana mzuri, aliyesimama pale akitazama huku na huko, lakini hakuweza kuyaona. Hakika. Baadhi yao wamejaliwa kuona, na wengine wasione. Na hiyo ni kweli.

²⁸⁰ Lakini sasa nyinyi ambao hamjawahi kuiona, hamjawahi kuiona, na nyinyi ambao mliiona kwa jicho lenu la kawaida na hamjawahi kuiona ile picha, hata ingawa wale waionao ile picha wanalo thibitisho kubwa zaidi kuliko ninyi ambao mmeiona kwa jicho lenu la kawaida. Kwa sababu nyinyi, kwa jicho lako la kawaida, mngeweza kukosea, ingeweza kuwa kiini macho. Hiyo ni kweli? Bali Hiyo si kiini macho, Hiyo ni ile Kweli, ambapo uchunguzi wa kisayansi unathibitisha ya kwamba Hiyo ni ile Kweli. Kwa hiyo Bwana Yesu ametenda hili.

"Unafikiria Hiyo ni nini basi," unasema, "Ndugu Branham?"

²⁸¹ Ninaamini ya kwamba ni Nguzo ile ile ya Moto ambayo iliwaongoza wana wa Israeli kutoka Misri hadi Palestina.

Ninaamini ni Malaika yule yule wa Nuru aliyekuja ge—gerezani na akamwendea Mtakatifu Petro na kumgusa, na akaenda mbele na kufungua mlango na kumtoa nje kwenye mwanga. Pia nasadiki ya kwamba ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina! Ni Yesu yeye yule leo ambaye alikuwa jana. Atakuwa daima Yesu yule yule.

²⁸² Na wakati ninapozungumza juu ya Hiyo, Nuru iyo hiyo ambayo iko kwenye picha iko kwenye . . . imesimama si futi mbili kutoka ambapo ninasimama sasa hivi. Hiyo ni kweli. Siwezi kuiona kwa ma—macho yangu, lakini najua imesimama hapa. Najua inatulia ndani yangu sasa hivi. Loo! Kama ungeweza tu kujua tofauti wakati nguvu za Mungu Mwenyezi zinaposhika, na jinsi mambo yanavyoonekana tofauti!

²⁸³ Hiyo ni changamoto, mtu yeyote. Sikuwa ninaenda kuwaombea wagonjwa wowote, nilikuwa ninaenda kufanya ahadi. Bali ono linaning'inia juu ya watu. A-ha. Mungu anajua hilo. Sitaitisha mstari wowote wa maombi, nitawaacheni tu mketi hapo. Ni wangapi wenu nyinyi watu wasio na kadi ya maombi? Hebu tuone mkono wako, mtu fulani ambaye hana kadi ya maombi, asiye na kadi ya maombi.

²⁸⁴ Mama mweusi anayeketi hapa, naona uliinua juu mikono yako. Hiyo ni kweli? Simama tu ili niweze kukutofautisha tu kwa dakika moja. Sijui kile Roho Mtakatifu atakachosema, lakini unaniangalia kwa unyofu kabisa. Huna kadi ya maombi? Kama Mwenyezi Mungu atanifunulia kilicho shida yako . . . Ninafanya hili tu kwa kuanzia, kupata tu kuanza. Unaniamini mimi kuwa . . . Unajua hakuna kitu . . . hakuna kitu kimoja kizuri kunihusu mimi. Kama wewe ni mwanamke uliyeolewa, mimi si zaidi ya mume wako. Mimi ni mwanamume tu. Lakini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na Yeye alimtuma Roho Wake kuthibitisha mambo haya.

²⁸⁵ Kama Mungu ataniambia shida yako (na wewe unajua ya kwamba hakuna njia kwangu mimi kuwa na mawasiliano na wewe hata kidogo), utaamini kwa moyo wako wote? [Dada huyo anaelezea—Mh.] Mungu akubariki. Basi shinikizo lako kuu la damu limekuacha. Hiyo ndiyo uliyokuwa nayo. Hiyo si ilikuwa kweli? Basi keti chini.

²⁸⁶ Hebu liamini tu hilo wakati mmoja! Ninamsahi mtu yeyote kuamini Hilo.

²⁸⁷ Angalia hapa, hebu niwaambieni jambo fulani. Martha, akija kwa Bwana Yesu. Kipawa hicho kisingefanya kazi hata kidogo . . . Baada ya Baba kuwa amekwisha kumwonyesha Yeye kile alichokuwa anaenda kufanya. Kisingelifanya kazi. Lakini alisema, “Bwana, mimi . . . Kama Wewe ungalikuwepo hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Kasema, “Lakini ninajua kwamba hata sasa lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

288 Akasema, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima, yeye aniaminiye Mimi ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na yeyote aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kabisa. Je! unasadiki hayo?”

289 Sikilizeni yale aliyosema. Alisema, “Naam, Bwana. Mimi nimesadiki ya kwamba kila jambo ulilosema Wewe ni Kweli. Ninaamini Wewe ndiwe Mwana wa Mungu yule ajaye ulimwenguni.” Huko ndiko kukaribia kwake, kwa unyenyekevu.

Unajisikia tofauti, sivyo, mama? Naam. Hiyo ni kweli.

290 Maskini mama huyo anayeketi hapo hapo, hapo kando yako, pia, ana ugonjwa wa baridi yabisi na shida ya kike. Hiyo si ni kweli, mama? Hebu simama kidogo tu, maskini huyo mama mwenye nguo nyekundu. Ulikuwa karibu sana, hilo ono limekuja kwako. Baridi yabisi, shida ya kike. Je! hiyo ni kweli? Na hapa kuna kitu katika maisha yako (una—una kitu kilichokukazia macho moja kwa moja): una mahangaiko mengi sana maishani mwako, shida nyingi sana. Na shida hiyo inamhusu mpendwa wako, ni mume wako. Ni mlevi. Hataki kwenda kanisani. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mungu akubariki, mama. Nenda nyumbani sasa na upokee baraka yako. Umeponywa, inaangaza nuru kukuzunguka.

291 Mwanamume aliyeketi moja kwa moja kando yako hapo. Wewe, bwana, unaamini? [Ndugu huyo anasema, “Naam. Ninaamini.”—Mh.] Kwa moyo wako wote? [“Naam, bwana.”] Umpoteza moja ya hisi zako. Hiyo ni hisi ya kunusa. Hiyo si ni kweli? Kama ni kweli, pungu mkono wako. [“Hiyo ni kweli.”] Weka mkono wako kinywani mwako, namna *hii*, useme, “Bwana Yesu, ninakuamini kwa moyo wangu wote.” [“Bwana Yesu, ninakuamini kwa moyo wangu wote.”] Mungu akubariki. Enda sasa. Utapokea uponyaji wako.

292 Mwaminini Mungu! Nyinyi nyote mnafikiria nini kuhusu Hilo, huko nyuma? Mnaamini? Iweni na kicho!

293 Yupo mama mmoja anayeketi moja kwa moja nyuma kule pembeni. Naiona hiyo Nuru ikining’inia juu yake. Hivyo ndivyo tu ninavyoweza kujua chochote kuihusu, Nuru hiyo inaning’inia. Nuru *Hii* papa hapa inaning’inia juu ya huyo mama. Labda katika dakika moja tu, kama ninaweza kuona ni kitu gani. Itavunja... Huyo mama anaugua—anaugua ugonjwa wa moyo. Ananiangalia mimi moja kwa moja.

294 Na mume wake ameketi karibu naye. Na mume wake ana maradhi fulani, amekuwa tu mgonjwa, ana fadhaa, mgonjwa. Hayo si ni kweli, bwana? Inua mikono yako juu kama hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, ni wewe, mama, uliye na skafu ndogo hapo. Huyo bwana, hiyo si ni kweli? Hivi si umekuwa tu na fadhaa kwa namna fulani leo? Umechafukiwa na tumbo lako, huyo mwanamume. Hiyo ni kweli.

295 Nyote mnaamini kwa moyo wenu wote, nyote wawili? Mnalikubali Hilo? Bwana, nakwambia, wewe pia, ninakuona

umeinua mkono wako, tabia ya kuvuta sigara. Acha kufanya jambo hilo. Unavuta sigara, si vizuri kufanya hilo, inakufanya mgonjwa. Hiyo si ni kweli? Kama ni kweli, pungu mkono wako namna hii. Hicho ndicho kinachokuchefua. Ni kitu kibaya kwenye mishipa yako. Tupa hicho kitu kibaya na usitende hilo tena, nawe utavuka jambo hilo na uwe mzima, na ugonjwa wa moyo wa mke wako utamwacha. Unaamini hilo? Hiyo si ni kweli? Siwezi kukuona kutoka hapa, na wewe unajua hilo, lakini unabeba sigara kwenye... kwenye—kwenye mfuko wako wa mbele. Hiyo ni kweli. Toa vitu hivyo kisha uweke mkono wako juu ya mke wako, mwambie Mungu ya kwamba umeachana na takataka za namna hiyo, utaenda nyumbani mzima, wewe na mke wako mtapona. Jina la Bwana Yesu libarikiwe!

Mnaamini kwa moyo wenu wote?

²⁹⁶ Maskini mama huyu anayeketi hapa akinitazama hapa. Wewe uliye kwenye...hapo kwenye kiti cha mbele hapa, unayeketi papa hapa. Maskini mama aliye na...akinitazama, akiketi papo hapo. Huna... Una kadi ya maombi, mama, papa hapa? Huna kadi yoyote ya maombi? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini kwamba Yesu Kristo anaweza kukuponya?

²⁹⁷ Unafikiri nini kuhusu Hilo, wewe unayeketi karibu naye? Je! una kadi ya maombi, mama? Huna? Unataka kupona, pia? Hivi si ungetaka kwenda kula tena kama ulivyozeo kufanya, shida ya tumbo iishe? Unaamini Yesu anakuponya sasa? Simama kama unaamini Yesu Kristo alikuponya. Ulikuwa na tumbo lenye vidonda, sivyo? Limesababishwa na hali ya fadhaa. Umekuwa na fadhaa kwa muda mrefu. Zaidi sana asidi na kadhalika, ama ninamaanisha inafanya asidi, na kuyafanya meno yawashe unapopiga mbweu chakula kikarudi kinywani mwako. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Ni kidonda cha tumbo, kilikuwa kipo chini kwenye tumbo lako. Huwasha wakati mwingine baada ya kula hasa tosti yenye siagi. Kweli? Sisomi akili zako, bali Roho Mtakatifu hakosei. Umeponywa sasa. Nenda nyumbani, upate afya.

²⁹⁸ Mnafanya nini nyuma huko upande huu? Baadhi yenu huko bila kadi ya maombi, inua mkono wako. Mtu fulani asiye na kadi za maombi. Sawa, iweni na kicho, amini kwa moyo wako wote. Vipi kuhusu huko juu kwenye roshani? Mwaminini Mungu.

²⁹⁹ Siwezi kutenda jambo hili mimi mwenyewe, ni neema Yake kuu tu. Unaamini? Naweza tu kutamka kadiri Yeye anavyonionyesha. Kama imani yako...Nasema hilo kuitikisa imani yako, halafu nione ataniongoza njia ipi. Je! mlitambua huyu—huyu si ndugu yenu? Mnasimama katika Uwepo Wake. Si mimi ninayetenda jambo hili, ni imani yenu inayoendeleza jambo Hili. Mimi siwezi kuliendeleza. Ni imani yenu ndiyo inayofanya jambo hili. Sina njia ya kuliendeleza. Hebu kidogo.

³⁰⁰ Katika kona hii namwona mtu mweusi ameketi pale, ni mzee kidogo, amevaa miwani. Una kadi ya maombi, bwana? Simama kwa miguu yako kwa dakika moja. Unaniamini mimi kwamba ni mtumishi wa Mungu, kwa moyo wako wote? Unafikiria juu ya mtu mwingine, sivyo? Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Si kwa sababu ni mimi, ndugu yako. Sasa, huna kadi ya maombi. Hakungekuwa na njia yoyote kwako wewe kuingia kwenye mstari, maana huna kadi ya maombi. Sasa, kama yeyote wenu ana kadi za maombi, msi—msi—msiinuke, mnaona, maana mtapata nafasi ya kuja kwenye mstari.

³⁰¹ Lakini ninaona Nuru hiyo ikiwa inaning'inia tu juu yake. Haijaingia kwenye ono bado. Siwezi kukuponya, ndugu, siwezi. Mungu tu ndiye anayeweza kufanya jambo hilo. Lakini wako. . . ninii yako. . . unayo imani. Unaamini. Na kuna kitu—kitu fulani, ambacho—ambacho kimeisababisha, kwa njia fulani.

³⁰² Kama Mwenyezi Mungu atamwambia mtu huyu shida yake ni nini, je! nyinyi wengine mtapokea kuponywa kwenu? Yupo mtu, amesimama kabisa yadi kumi, kumi na tano mbali na mimi, sijawahi kumwona maishani mwangu. Ni mtu tu anayesimama hapo. Kama Mwenyezi Mungu atafunua shida aliyo nayo mtu huyu, kila mmoja wenu anapaswa kutembea kutoka hapa akiwa mtu mzima. Mungu anaweza kufanya nini zaidi? Hiyo ni kweli?

³⁰³ Bwana, huna shida yoyote. U mnyonge, unaamka kidogo usiku, tezi dume na kadhalika, lakini hiyo siyo iliyo shida yako. Shida yako ni kuhusu mvulana wako. Na mvulana wako yuko kwenye namna fulani ya hospitali ya serikali, naye ana hulka mbili. Hiyo ni kweli? Punga mkono wako kama hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

³⁰⁴ Ni wangapi wanaamini sasa kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu anasimama hapa? Hebu tusimame na kusifu na tupokee uponyaji wetu.

³⁰⁵ Mungu Mwenyezi, Mwanzilishi wa Uhai, Mpaji wa kila kipawa chema, Wewe upo hapa, Bwana Yesu Kristo yule yule, yeye yule jana, leo, na hata milele.

³⁰⁶ Basi, Shetani, umewadanganya watu hawa muda mrefu vya kutosha, toka ndani yao! Nakuapisha kwa Mungu aliye hai ambaye Uwepo Wake upo hapa sasa katika umbo la Nguzo ya Moto, waache watu hawa! Na utoke ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo!

³⁰⁷ Kila mmoja wenu inueni mikono yenu na mumsifu Mungu, na mpokee uponyaji wenu, kila mmoja. [Kusanyiko linamsifu Mungu—Mh.]



JINSI YULE MALAIKA ALIVYONIJIA, NA AGIZO LAKE SWA55-0117

(How The Angel Came To Me, And His Commission)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu, tarehe 17 Januari, 1955, katika Shule ya Sekondari ya Juu ya Lane Tech kule Chicago, Illinois, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org